Ijumaa Aprili 10, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580202

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710



## Mwalimu mkuu auawa kikatili, mwili wake watupwa shambani

UKURASA 2


Corona ilivyozaa maisha mapya ndani ya biashara

BUFE

Ijumaa Aprili 10, 2020 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Vijana Mwanza walivyowekeza katika sanaa na kuonyesha maana ya ajira

BIASHARA

Na Gwamaka Alipipi

Tabasamu la Wabunge kwa wazalisha umeme

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati, Dustan Kitandula (kushoto kwake), wakipata maelezo kutoka kwa mfanyakazi wa kiwanda cha Africab, David Tarimo. Wa kwanza kulia, ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Mansoor Moiz. PICHA; MAKTABA

UKURASA 11

# HOFU CORONA



## Serikali yatoa tahadhari maambukizi ya ndani

**WAZIRI** asema maambukizi ya wenyewe kwa wenyewe yameanza, mwongozo mpya waja...

*Endelea ukurasa 2*

## TAKUKURU YAFICHUA WASTAAFU KUTAPELIWA NA WAKOPESHAJI

UKURASA 2

## Mabasi ya Mwendokasi yalivyonunuliwa kifisadi

UKURASA 4

### BAA LA CORONA



"Ugonjwa huu unaambukiza sasa hivi kwa njia ya hewa, hii ni kwa mujibu wa takwimu mpya, wataalamu watatoa taarifa, tutatoa mwongozo ndani ya siku mbili au tatu kwa jamii kuhusu uvaaji wa barakoa." Ummy Mwalimu.

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo


Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store

MICHEZO **MIHAYO AWATAKA SIMBA KUZINDUKA** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Takukuru yafichua wakopeshaji kuwatapeli wastaafu

**Na Enock Charles**

MKURUGENZI wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Bregedia John Mbungo, amesema wamebaini utapeli wa kutisha kwa walimu na wastaafu unaofanywa na vikundi vya ukopeshaji.

Pia, alisema Takukuru itaendelea kupambana na wakopeshaji wa mitaani ambao wanawabambikiza watumishi hasa walimu, kwa riba kubwa kupita kiasi na ambazo kisheria hazikubaliki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi huyo alisema taasisi hiyo haitakivumilia kikundi chochote chenye mikopo inayowaumiza wananchi na watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Uchunguzi wa Takukuru umebaini kuwa waathirika wakubwa wa uwapo wa kikundi hicho ni wastaafu na hususan walimu," alisema.

Kwa mujibu wa Bregadia Mbungo, mstaafu mmoja alikopa Sh. 900,000 aliyetakiwa kulipa Sh. 1,260,000 kwa riba ya asilimia 40 ambayo bado iko juu, lakini alilazimika kulipa Sh. milioni 12,500,000, sawa na riba ya asilimia 300.

Alisema mstaafu mwingine mwingine alikopa Sh. milioni tano, ambayo alitakiwa kulipa Sh. milioni saba kwa riba ya asilimia 40, lakini alilipa Sh. milioni 20 sawa na riba ya asilimia 300.

Vile vile, alisema kwa Mkoa wa Mara pekee, hadi kufikia Aprili mwaka huu, taasisi hiyo ilifanikiwa kuwarejeshea wastaafu fedha walizokuwa wameporwa kiasi cha Sh. milioni 289 pamoja na nyumba ya mjane yenye thamani ya Sh. milioni 40.

Alitaja urejeshaji wa fedha hizo uliofanywa na vikundi hivyo na idadi ya fedha kwenye mabano ni Tabora (milioni 41.2), Katavi (milioni 29), Mwanza (milioni 17.4), Kagera (milioni 10), Njombe (milioni 5) huku Rukwa akikamata mkopeshaji mwenye kadi 85 za benki.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamabana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbungo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mikakati waliyojiwekea katika mwaka huu wa 2020/2021, ikiwa ni pamoja na kujipanga kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yatoa tahadhari maambukizi ya ndani

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema maambukizi ya virusi vya Corona Tanzania sasa ni ya ndani ya nchi na muda mfupi yatakwenda kwenye kijamii.

Amesema mgonjwa mmoja mwanaume mwenye umri wa miaka 51 aliyebainika jana na mwingine juzi mwanaume mwenye umri wa miaka 41, ni wa ndani nchi. Waziri Ummy alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa madhehebu ya dini kitaifa kuhusu virusi vya Corona. Alisema Tanzania imetoka katika hatua ya maambukizi ya kutoka nje ya mipaka hadi ndani ya nchi.

"Tumetoka kwenye maambukizi yanayoletwa kutoka nje ya nchi, tuko kwenye maambukizi ya ndani, takwimu za kesi za jana na juzi tumeanza kuambukizana wenyewe kwa wenyewe," alisema.

"Tumeanza kuambukizana wenyewe kwa wenyewe, hili lazima niliweke wazi, hatuna kesi za kutoka nje ya mipaka, tumeanza maambukizi ya ndani, ya siku chache tutaingia kwenye maambukizi ya kwenye jamii.

"Maana yake, tutapata mgonjwa halafu hatutajua amepata wapi maambukizi, amekuja mtu anamwambukiza mwingine, ndiyo maana tumejielekeza kuwatafuta na kuwabaini washukiwa."

"Sasa tukishatoka hapo, utampata mtu, hujui ameambukizwa na nani, ndani ya siku chache tutaweza kuingia katika hatua hiyo lazima niwaambie ukweli, tunahitaji kuongeza jitihada zaidi."

Waziri Ummy alisema kikubwa ni watu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima na ibada ziendeshwe kwa namna ambayo siyo hatarishi. "Wataalamu wanasema angalau umbali usiopungua mita moja kati ya mtu na mtu, tupaswa kuangalia je, kuna haja ya kufanya mkusanyiko kama huu?.

"Ninachotaka kusema, makongamano ya dini hapana katika kipindi hiki, nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani, kuna watu walitaka kufanya kongamano la watu 3,000 nikamwambia hapana."

Pia, aliwaomba viongozi wa dini kadiri inavyowezekana, wafanye ibada kwa kutumia muda mfupi.

"Tunategemea mtatoa miongozo kuhusu utoaji wa huduma za kiroho kwa wagonjwa, ndugu na marehemu, tunahitaji muendelee kutoa huduma hizo, lakini mjue mpo katika kipindi cha mlipuko."

**CORONA YAAMBUKIZWA KWA HEWA**

"Ugonjwa huu unaambukiza sasa hivi kwa njia ya hewa, hii ni kwa mujibu wa takwimu mpya, wataalamu watatoa taarifa, tutatoa mwongozo ndani ya siku mbili au tatu kwa jamii kuhusu uvaaji wa barakoa.

"Hadi sasa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) linasema wanaotakiwa kuvaa ni wale wanaotoa huduma, wagonjwa na walio katika maeneo hatarishi, kwa sababu kuna tathmini kwamba tunaweza kupata kwa njia ya hewa."

**KILA MTU KUVAA BARAKOA**

"Tunatafakari ndani ya siku mbili au tatu tutatoa mwongozo kila mtu akitoa nje ya nyumba yake au sehemu ya watu wengi avae barakoa."

Waziri Ummy Pia, aliwataka viongozi wa dini kuwaambia ukweli waumini wenye dalili za kikohozi, mafua na homa wabaki nyumbani badala ya kwenda kwenye nyumba za ibada.

Kadhalika, aliwataka wananchi kujiuliza katika kipindi hiki cha sikukuu, kama upo ulazima wa kwenda kusalimia kijijini.

**AKEMEA WATOTO KUZURURA**

"Shule zimefungwa, lakini watoto wanazurura mtaani, imekuwa kipindi cha kwenda kwa mjomba, shangazi tunatakiwa kuwalinda na kuwakinga watoto wetu," alisema.

Alisema kituo cha Udhibiti wa Magonjwa Barani Afrika, takwimu zake zinaonyesha wapo wagonjwa takriban 10,000 na vifo takriban 500 barani Afrika.

**TAKWIMU ZA WHO**

Ummy alisema WHO iliikadiria Tanzania ifikapo katikati ya mwezi huu itakuwa na wagonjwa 1,000.

"Wakija 10,000 kati yao, asilimia 80 hawataumwa sana bali asilimia 20 watahitaji kulazwa, je tuna maeneo ya kutosha, tunafikiria na tunapanga mipango. Msikubali kukutana na watu bila sababu za lazima mnaweza kutumia mkutano kwa njia ya video.

"Tumefanya makadirio ya Afrika nzima itakapofika katikati ya mwezi Mei tutakuwa na wagonjwa 10,000, mpaka muda huu tumeshavuka kihunzi cha WHO."

**AWAANGUKIA VIONGOZI WA DINI**

Waziri Ummy alisema viongozi wa dini wana nafasi tatu za kusaidia kwa sababu wanaaminika na kukubalika na jamii katika kutoa maelezo, faraja na utoaji huduma za afya na kijamii za moja kwa moja.

**NYUMBA ZA IBADA HAZIJAFUATA MAELEKEZO**

Awali, Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema nyumba nyingi za ibada hazijafuata maelekezo yaliyotolewa na serikali hivyo wanagemea kupata mwongozo.

"Tunamshukuru Rais John Magufuli alisema wazi nyumba za ibada zisifungwe limetufariji sana na kutupa moyo wa kumlilia Mungu zaidi."

# Mwalimu mkuu auawa kikatili

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI La Polisi Mkoa wa Dodoma, linawashikilia watu watano kwa tuhuma za mauaji ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chilungulu, Wilaya ya Bahi, Eradius Mgaya(41) na kumtupa kwenye shamba la shule.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 7, mwaka huu katika kijiji cha Chilungulu.

Alisema mwalimu huyo alipigwa kitu chenye ncha kali na kutupwa kwenye shamba la shule.

"Hawa watuhumiwa walimvizia njiani alipokuwa akirejea nyumbani kwake...bado tunachunguza chanzo cha kifo, na watuhumiwa tunawashikilia hadi hapo tutakapokamilisha uchunguzi," alisema. Hata hivyo, Muroto hakutaja majina ya watuhumiwa wa hao kwa maelezo kuwa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi.

Katika hatua nyingine, Mkazi wa Image Jiji la Dodoma, Godfrey Shirima (22), anashikiliwa kwa kukutwa na bastola yenye namba za usajili 016975 ambayo anamiliki kinyume na sheria huku akitumia katika uhalifu.

Alisema mtuhumiwa huyo anatarajiwa kufikishwa mahakamani upelelezi utakapo kamilika. Wakati huo huo, Kamanda huyo alionya mikusanyiko isiyo ya lazima itakayosababisha msongamano hasa wakati huu ambao kila raia anapaswa kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona.

## HABARI KITAIFA



Kamanda wa Polisi mkoa wa Shinyanga, ACP Debora Magiligimba, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, mali mbalimbali za wizi zilizokamatwa na jeshi hilo, katika misako mbalimbali mkoani humo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mbunge aishauri NEC kupitia upya ugawaji majimbo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nkasi Kaskazini (CCM), Ally Keissy, ameshauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ipitie upya ugawaji wa majimbo kutokana na baadhi yao kuwa na kata chache.

Akichangia jana Bungeni Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kwa mwaka 2020/21, Kessy alisema baadhi ya majimbo kuna kata sita huku mengine yana kata zaidi ya 30, lakini mgawo wa fedha za miradi hauzingatii ukubwa wa jimbo au wilaya.

"Kuna halmashauri zina kata tano au sita, kuna halmashauri kata nne au sita, zingine 28, halmashauri zingine zimegaiwa kisiasa, mpitie upya mgawo msifuate kwa halmashauri wa vituo vya afya, zahanati.

"Kwanini wapate vituo vya afya vitatu na maabara nane haiwezekani, lazima tufuate idadi ya kata, kuna wabunge walipewa majimbo na halmashauri kisiasa leo wanataka kupata mgwao kisiasa haiwezekani," alisema.

Alishauri Ofisi ya Tamisemi kupitia upya mgawo huo ili kuweka usawa.

Hata hivyo, alisema kuwa halmashauri inatakiwa kulipa posho ya madiwani kwa kutumia makusanyo yake ya ndani, huku akitaka ambazo zinashindwa kukusanya kwa vigezo vilivyowekwa kufutwa.

# Ataka fedha elimu bure zinunuliwe 'sanitizer'

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI baa la corona likiendelea kusababisha madhara duniani, baadhi ya wabunge wameitaka serikali kubadili matumizi ya fedha za Mpango wa Elimumsingi Bila Ada, maarufu elimu bure ili zitumike kununua vitakasa mikono (hand sanitizers) kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo.

Vilevile, baadhi ya watunga sheria hao wameitaka serikali kulieleza Bunge kiasi cha fedha kilichotumika katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita.

Hoja hizo ziliibuka bungeni jijini hapa jana wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika mjadala huo, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega (Chadema), aliitaka serikali kutoa taarifa bungeni kuhusu kiasi cha fedha kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya kufanikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba mwaka jana.

Alisema kutokana na vyama vya upinzani kujitoa kushiriki katika uchaguzi huo, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya uchaguzi huo, sasa zielekezwe kwenye masuala ya msingi.

"Ni kiasi gani kilichotengwa kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa? Maeneo mengi watu walipita bila kupingwa na chenji yetu irudi ili ikafanye mambo ya msingi.

"Kuna ahadi ilitolewa ya bajaj kama 'ambulance' (gari la wagonjwa). Na Sh. milioni 50 kila kijiji nazo hatujaziona katika halmashauri zetu ilhali (George) Simbachawene aliahidi hapa bungeni kwamba itatekelezwa katika awamu hii ya tano," alisema.

Mbunge huyo pia aliungana na wabunge wengine wengi walioitaka serikali kutenga fedha za ndani kwa ajili ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) badala ya kutegemea fedha za nje ambazo walitahadharisha kuwa mwaka huu huenda zisipatikane kutokana na mataifa mengi kuweka nguvu katika mapambano dhidi ya baa la corona.

Hoja hiyo ya Tarura kupewa kipaumbele iliungwa mkono na Mbunge wa Mchinga, Hamidu Bobali (CUF), ambaye pia aliitaka serikali kuhakikisha inalipa posho na stahiki za madiwani kabla ya Mei mwaka huu.

Kuhusu baa la corona, Bobali aliitaka serikali itumie fedha za Mpango wa Elimumsingi Bila Ada, kununua vitakasa mikono na kuzisambaza kwenye halmashauri ili zitumiwe na wanafunzi ambao kipindi hiki wako nyumbani baada ya shule zote kufungwa.

"Shule zimefungwa. Fedha za elimu bure kwa mwezi kila halmashauri ilikuwa inapata si chini ya Sh. 50 mil. Kwanini fedha hizo zisitumike kununua sanitizers na vifaa vingine kwa wanafunzi walioko huko majumbani kujikinga na corona?" Alihoji.

Seif Gulamali, Mbunge wa Manonga (CCM), aliipongeza serikali kwa kukarabati na kujenga hospitali za halmashauri, akiiomba iikumbuke Halmashauri ya Igunga kwa kuongeza majengo ya mama na mtoto na mochwari kwenye hospitali ya wilaya.


**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA**

TANESCO

**TAARIFA KWA UMMA**

**MKAKATI WA SHIRIKA KATIKA KUPAMBANA NA MAAMBUKIZI YA UGONJWA WA HOMA KALI YA MAPAFU INAYOSABABISHWA NA VIRUSI VYA CORONA (COVID-19)**

**APRILI 09,2020**

**Kufuatia tamko la Serikali kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya kuenea kwa maambukizi ya ugojwa hatari wa Corona (Covid-19)**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linapenda kuwafahamisha wateja wote na wananchi kwa ujumla, kuwa kufuatia mlipuko wa ugonjwa hatari a Corona, TANESCO itaendelea kufuata taratibu zote za kuchukua thadari zinazo tolewa na Wizara ya Afya kwa Kupunguza msongamano wa watu usio wa lazma katika ofisi zote za Shirika ili kuweza kuwakinga watumishi na maambukizi ya Corona.

**Ili kufanikisha maelekezo haya ya Serikali kwa ufanisi mkubwa TANESCO inawashauri wateja wetu katika kipindi hiki,**

Kutumia njia zetu mbadala za mawasiliano ikiwa ni pamoja na simu au barua pepe pamoja na mitandao ya kijamii na "**TANESCO app**", ili kufikisha matatizo maoni na maombi ya wateja kwa Shirika, na changamoto zozote za huduma wanazo pata ili zipatiwe utatuzi kwa wakati, hii itasaidia kupunguza msongamano wa wateja katika ofisi zetu.

Kwa wateja wote watakaolazimika kufika katika ofisi za shirika wanaombwa kuzingatia taratibu zote za kiusalama zilizowekwa katika ofisi zetu ikiwemo kunawa mikono kwa kutumia vitakasa mikono (sanitizers) vilivyowekwa katika kila ofisi, kabla ya kuingia katika ofisi husika na wakati wa kutoka.

Wateja wote watakaofika katika ofisi za Shirika watalazimika kufuata utaratibu maalum ulio wekwa eneo la mapokezi. ikiwa ni pamoja na kutoruhusiwa kuingia katika ofisi za Shirika na inapobidi basi Mfanyakazi ataonana na mgeni katika eneo la nje ya ofisi za Shirika na itawalazimu kuzingatia umbali (physical distancing ) unao shauriwa ikiwa ni angalau kukaa umbali wa mita moja kutoka kati ya mteja na mtoa huduma .

TANESCO itaendelea kuchukua hatua zote muhimu za tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Corona bila kuathiri utendaji wa kazi za Shirika na utoaji huduma kwa wateja wetu. TANESCO inawashukuru kwa ushirikiano wenu.

**Imetolewa na: Ofisi ya Uhusiano**
**TANESCO-Makao Makuu**

# Mabasi ya Mwendokasi yalivyonunuliwa kifisadi

## ■CIG abaini ulaji wa kutisha, vigogo walipwa mabilioni kiajabu



**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2018/19, imebaini kuwapo kwa ufisadi katika ununuzi wa mabasi, vipuli na usimamizi wa mali za kudumu kwenye Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, maarufu mwendokasi.

Katika ripoti yake kuhusu mashirika ya umma, CAG Charles Kichere (pichani), anabainisha upigaji wa mabilioni ya shilingi katika mradi huo baada ya kukagua hesabu za Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA/UDART).

Anasema kuwa Kampuni ya Mabasi ya yaendayo haraka (Rapid Transit) ilianzishwa Desemba 19, 2014 na kumilikiwa na UDA kwa asilimia 99 na Kampuni ya Simon Group Limited kwa asilimia moja.

Kufuatia makubaliano kati ya serikali na Kampuni ya Simon Group Ltd ya Oktoba 9, 2019, CAG anasema Shirika la UDA likamiliki Kampuni ya UDART kwa asilimia 100 huku Shirika la UDA likimilikiwa na serikali kwa asilimia 85 na Kampuni ya Simon Group Limited kwa asilimia 15.

CAG anasema Mei 14, 2019, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, aliiomba ofisi yake kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi katika UDA na kampuni tanzu ya UDART juu ya ununuzi wa mabasi na vipuli, uingiaji na usimamizi wa mikopo, ununuzi ya hisa za kampuni, usimamizi wa mali za kudumu zisizohamishika zilizokodishwa na uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa 2016) na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (marejeo ya 2016) kwenye usimamiaji wa mikataba.

Anasema ukaguzi huo ni mwendelezo wa ukaguzi uliofanyika mwaka jana na kubaini upungufu kwenye nyanja tofauti ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mabasi kwa bei ya kuongezwa Dola za Marekani milioni 14.41 (Sh. bilioni 33.179).

"UDART na UDA walisaini mikataba mitatu kati ya Oktoba 10, 2014 na Julai 15, 2015 na Kampuni ya Xiamen Golden Dragon Bus Co. Ltd (muuzaji) kwa ajili ya ununuzi wa mabasi ya mwendokasi 140. Hadi kufikia Agosti 24, 2015, mabasi 138 yalikuwa yamewasili na kupokewa katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Mabasi haya yalipokewa yakiambatana na hati tatu za malipo, ambazo ni GDES-15-156A kwa mabasi 56, GDES-15-156B kwa mabasi 28, na GDES15-252 kwa mabasi 54, zote zikiwa za Agosti 24, 2015," anasema.

CAG anasema ukaguzi wake ulibaini kuwa kulingana na kifungu cha mkataba wa huduma baada ya mauziano (after sales services) kwa mabasi 84 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 13.37, muuzaji atatoa bila malipo vipuli vya mabasi vyenye thamani sawa na asilimia mbili (Dola za Marekani 267,425) ya mauzo kwa muda wa miezi 36 kupitia Kampuni ya Simon Motors Ltd ambayo ni wakala wa muuzaji.

"Nilibaini kuwa vipuli vyenye thamani ya Dola za Marekani 99,467 (Sh. milioni 229.181) pekee ndivyo vilitolewa kwa UDART huku vipuli vilichobaki vyenye thamani ya Dola za Marekani 167,958 (Sh. milioni 386.99) vikiwa bado havijatolewa na wakala.

"Ukaguzi juu ya hati za malipo uligundua kuwa bei za mabasi kwenye hati za malipo (Dola za Marekani milioni 11.24) zilizotumwa Mamlaka ya Mapato (TRA) na Bandari ya Dar es Salaam, zilikuwa za chini ikilinganishwa na bei ya mkataba wa mauziano uliokuwa na Dola za Marekani milioni 25.65.

"Hata hivyo, Mwenyekiti Mtendaji aliielekeza Menejimenti ya UDART kumlipa muuzaji kwa bei ya mkataba ambayo ni kubwa na hivyo kampuni kufanya malipo ya juu kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 14.41.

"Pia, kutokana na viashiria na mwendelezo wa matukio, inaonekana malipo ya ziada ya Dola za Marekani milioni 14.41 yalitumiwa na Kampuni ya Simoni Ground Limited kununua mabasi mapya 70 kwa mkataba ulioingiwa Septemba 30, 2017 kwa bei ya Dola za Marekani milioni 17.68.

"Mabasi hayo yalihamishiwa kwenye Kampuni ya UDART na Kampuni ya Simon Group Limited kwa bei ya Dola za Marekani milioni 20.33, ikimaanisha kuwa Kampuni ya Simon Group limited ilipata faida ya Dola za Marekani milioni 2.65 kutokana na muamala huu na ilikubalika kuwa malipo yatafaywa na UDART baada ya mabasi kuanza kutumika," anainisha.

CAG Kichere anaendelea kufichua kuwa kampuni za Simon Group Limited na UDART hazikuwasilisha taarifa katika Mfumo wa Forodha (Tancis) wa TRA juu ya uingizaji wa mabasi hayo na matokeo yake, mabasi yanashikiliwa na mamlaka hiyo kwa zaidi ya siku 721 (Februari 2018 hadi Februari 2020) na yana deni la Dola za Marekani milioni 2.3 kama gharama za utunzaji katika maghala yake.

CAG anaishauri Menejimenti ya UDART iiagize Kampuni ya Simon Motors kukabidhi vipuli vya huduma baada ya mauzo vilivyosalia; iombe kurejeshewa nyongeza ya bei ya ununuzi wa mabasi 138 au ikabidhiwe mabasi 70 yaliyohamishwa na Kampuni ya Simon Group Limited bila ya malipo; na ichukue hatua stahiki za kisheria dhidi ya Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya UDART kwa kuisababishia Kampuni ya UDART kufanya malipo ya juu katika ununuzi wa mabasi.

**UDANGANYIFU MALIPO MABILIONI**

Ripoti hiyo iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumatatu, inabainisha kuwa ukaguzi wa malipo yaliyofanywa na Kampuni ya UDA wakati wa utekelezaji wa mradi wa mabasi ya mwendokasi ulibaini ubadhilifu wa mabilioni.

CAG anabainisha kuwa mnamo Juni 18, 2015, Shirika la UDA na Kampuni ya UDART waliingia mkataba na kampuni mbili za Consultant for Resources Evaluation Limited na Enterprise Growth Market Advisors Limited kwa pamoja zikiitwa 'consortium' uliohusu kazi za kutangaza hisa za mtoa huduma wa Mradi wa Mabasi ya Mwendokasi katika soko la hisa la Dar es Salaam.

Anaendelea kubainisha kuwa mnamo Oktoba 8, 2015, UDART ilifanya malipo ya kiasi cha Sh. milioni 550 kutoka akaunti Na. 20110017710 DART PROJECT kwenda akaunti Na. 01J1027103201 ya Kampuni ya Consultant for Resources Evaluation Limited kwa ajili ya kutangaza hisa za awali.

"Hata hivyo, ilibainika kuwa siku hiyo hiyo ya Oktoba 8, 2015, Kampuni ya CORE Securities Ltd ilihamisha kiasi cha Sh. milioni 500 kwenda akaunti Na. 3004211129958 ya Shirika la UDA katika Benki ya Equity, taarifa ya benki zinaonyesha kuwa Ofisa Fedha wa UDA alitoa kiasi cha Sh. milioni 442 kama fedha taslimu bila ya maelezo stahiki.

"Pia, uhakiki kutoka Mamlaka ya Soko la Hisa na Mitaji (CMSA -Capital Market & Securities Authorities), umeonyesha kuwa mamlaka hiyo haikuwahi kupokea maombi ya kuuzwa kwa hisa za UDART katika Soko la Hisa na Mitaji. Hii inathibitisha kuwa Kampuni ya UDART haikuwa na nia ya kuuza hisa zake. "Katika uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayo kasi, Kampuni ya UDART ilisaini mkataba na Kampuni ya Kapsch CarrierCom Belgium NV (KCC) kwa ajili ya kuweka mfumo wa Tehama wa usafirishaji (Intelligent Transportation System (ITS)) na katika kutekeleza mradi huo, Kampuni ya KCC iliingia makubaliano ya ushirikiano na Kampuni ya Maxicom Africa Ltd kuwa wakala wake.

"Uchunguzi wangu ulibaini kuwa kuanzia Novemba 16, 2015 hadi Januari 5, 2016, Kampuni ya UDART ilikuwa imeilipa Kampuni ya Maxicom Africa Ltd jumla ya Sh. bilioni 3.91 kutoka akaunti Na. 20110017710 ya NMB (DART Project) kwenda akaunti Na. 10160168505 ya Maxcom Africa Ltd International Commercial (ICB), ambapo kiasi cha Sh. biilioni 3.48 ni kwa ajili ya usimikaji wa mfumo wa Tehama wa ITS, ununuzi wa kadi za wasafiri, na kufanya uwekezaji wa mifumo ya umeme wa dharura ingawa hakukuwa na mkataba kati ya UDART na Maxicom kuhusinana na malipo hayo.

"Pia, nilibaini kiasi cha Sh. bilioni 3.45 kilihamishwa kutoka akaunti Na. 10160168505 ya Maxcom Afrika Ltd kwenda katika akaunti binafsi Na.10160214306 katika Benki ya Kimataifa ya Biashara (International Commercial Bank) ya Mwenyekiti Mtendaji wa UDART ikisemekana kuwa fedha hizo zitatumika kulipia fidia na hisa kwa wamiliki wa daladala.

"Ninaishauri Menejimenti ya UDART ichukue hatua stahiki za kisheria dhidi ya Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya UDART pamoja na Mhasibu wa UDA kwa udanganyifu uliopelekea ubadhilifu wa fedha," CAG anapendekeza.

**Itaendelea kesho.**

# Serikali kujenga kituo cha magonjwa mlipuko

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema itajenga kituo cha kisasa cha kutolea huduma ya magonjwa ya mlipuko, kitakachogharimu zaidi ya Sh. bilioni 7, kitakacholaza wagonjwa 200.

Kituo hicho kitajengwa eneo la Kiloka karibu na Hospitali ya Mloganzila jijini Dar es Salaam.

Hayo yalielezwa katika taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, wazee na Watoto iliyotolewa jana, wakati Meneja mradi wa ujenzi wa kituo hicho, Solomoni Shausi, akizungumza na Makatibu wakuu 14 ambao ni wajumbe wa kamati ya kitaifa ya kupambana na virusi vya Corona (COVID-19), na kusema ujenzi unaofanywa na kikosi cha Suma (JKT), utakamilisha baadhi ya majengo ifikapo Aprili 30, mwaka huu.

Alisema jeshi limepeleka nguvu kazi ya wanajeshi 389 wanaojenga kituo hicho chini ya Suma JKT inayotakiwa kukamilisha ujenzi huo baada ya miezi sita kuanzia sasa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Zainab Chaula, alisema kituo hicho kitakapo kamilika, kitatumika kuhifadhi wagonjwa na wahisiwa wa ugonjwa wa mlipuko ukiwamo corona.

"Serikali imeamua kujenga kituo hicho na kitakapo kamilika kitakuwa cha aina yake nchini, kwani kitawekwa vifaa vya kisasa vya kurahisisha kutoa huduma kwa wagonjwa wa milipuko nchini," alisema.

Aidha, ujumbe ulifanya ziara ya siku moja ya maeneo kama hosteli ya Magufuli zinazoweka karantini wasafiri walioingia Dar es Salaam kutoka nje ya nchi, kituo cha matibabu ya wagonjwa wa corona kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani na kituo cha muda kilichopo Kisoka Mloganzila.

Mkuu wa kituo cha Kisoka, Dk. Christopher Mzava, aliuambia ujumbe huo kuwa sehemu hiyo iliyotengwa kwa muda kwa ajili ya waathirika wa corona, ina uwezo wa kulaza wagonjwa 40.

Katibu Tawala wa mkoa wa Pwani, Theresia Mmbando, akitoa taarifa kwa ujumbe wa makatibu wakuu, alisema kituo cha wangonjwa wa corona kilichopo Kibaha kimekamilia na kina uwezo wa kulaza wagonjwa 40, huku kikiwa na vifaa vyote muhimu kwa matibabu zikiwamo mashine za kupumulia (ventilators), vitanda, magodoro na mashuka.

Naye, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, aliueleza ujumbe huo kuwa kituo cha karantini cha hosteli za Magufuli hadi Aprili 8 kilikuwa na wasafiri 226 walioingia jijini kutoka nje ya nchi, kati yao 72 waliruhusiwa kutoka, baada ya kukamilisha siku 14 za uangali-

# Chadema wamkalia kooni Kigwangala

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo(Chaema), kimeiomba serikali kuwachukulia hatua Mawaziri waliotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) kuisababishia serikali hasara. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Bara, Singo Kigaila, alisema kama ambavyo serikali ilimchukulia hatua aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, ndivyo ambavyo inapaswa kuwachukulia hatua ikiwamo kuwafikisha mahakamani Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala na wengine.

"Hawa Mawaziri tayari wameshailetea serikali hasara, wanaachwaje, mamlaka zilizowateua ziwaondoe na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria ili waulizwe ni kwa nini walifanya hivyo," alisema Kigaila.

"Kigaila apelekwe mahakamani akaulizwe kwa nini ametumia Sh. bilioni 2.583 bila idhini ya bunge wala Waziri wa Fedha."

Kigaila alisema kitendo cha Dk. Kigwangala kuchukua fedha hizo bila idhini ya Wizara ya Fedha na Bunge huenda amekuwa akifanya hivyo mara nyingi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano, Uenezi na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alisema wapo Mawaziri wengi ambao waliondolewa katika nafasi zao na kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na ripoti za CAG.

"Tumewahi kushuhudia Mawaziri wengi wakiondolewa kwenye nafasi zao kutokana na ripoti hizi za CAG, Kigwangala atakuwa si wa kwanza na asione kama anaonewa bali achukuliwe hatua kama ilivyokuwa kwa wengine waliopita," alisema Mrema

Kwa mujibu wa ripoti ya CAG, Sh. bilioni 2.583 zilitumika kwa ajili ya tamasha la Urithi Festival bila idhini ya Waziri wa Fedha wala Bunge, na ilichukuliwa kutoka miongoni mwa taasisi zilizo chini ta wizara hiyo.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuwakinge wahitaji na corona, wasaidiwe maji

**USAFI** wa mikono na mwili wakati huu wa kupambana na corona ni jambo linalotoa chan gamoto kwa mataifa yote duniani kuwekeza kwenye miradi ya maji na kujenga miundombinu ya usambazaji na kuyafikisha kwa wananchi.

Kila binadamu popote alipo duniani leo, anahitajika kunawa mikono mara kadhaa na maji yanayotiririka pamoja na sabuni kwa sekunde kadhaa ili kujilinda na maambukizi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo corona.

Hatua hiyo, huchukuliwa iwe nyumbani, ofisini, kwenye huduma kama hospitalini na popote kwenye shughuli za binadamu.

Kutokana na uhitaji huu wa maji ulioko leo duniani pote, ni jambo linaweza kuchukuliwa kuwa ndiyo huduma ya kwanza katika kukabiliana na corona.

Kwa hiyo mahitaji hayo kuanzia sasa yaziamshe serikali kuwekeza zaidi kwenye maji na kuyafikisha kwa watumiaji walipo kuanzia mijini hadi vijini kwa Tanzania.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), mwanadamu anahitaji angalau lita za maji kati ya 2.5 hadi tano kwa siku kwa ajili ya kunywa , yaani wanawake wanashauriwa kunywa lita 2.7 hadi wakati wanaume hushauriwa kunywa lita 3 kwa siku.

Hata hivyo, ufafanuzi zaidi unaeleza kuwa angalau kila binadamu anahitaji angalau lita 50 za maji kila siku kwa matumizi mbalimbali kuanzia kunywa kuoga , kunawa na kuosha vyombo na kufanya majukumu mengine.

Aidha, hicho ni kiwango cha chini mno kwani kuna wengine hutumia maji hata zaidi ya lita 100 kwa siku ikimaanisha kuwa ni wastani wa ndoo tano kama ni hapa nchini.

Ni wazi kuwa matumizi ya maji ni makubwa mno kwa wakati huu wa kukabiliana na corona na kwamba ni vyema hili likawa somo kwenye jitihada za kuongeza huduma za jamii si kwa Tanzania bali hata kwa mataifa mengine ya Afrika.

Ni wazi kuwa, kwa wakazi wa mijini suala la kunawa na kusafisha mikono ni jambo ambalo litaifanya huduma ya maji kuwa kubwa zaidi nchini kwa hiyo ni vyema wadau wanaochangia serikali kupambana na corona kuweka kipaumbele katika upatikanaji wa huduma za maji kwa watu mbalimbali walio kwenye maeneo mengi tofauti.

Wanaweza kusaidia juhudi hizo lwa kusimika matangi makubwa ya maji na kusaidia kufikisha maji kwenye sehemu mbalimbali zikiwa ni pamoja na vituo vya mabasi, hospitalini, kuanzia zahanati, vituo vya afya, hospitali za rufani, za kanda na Muhimbili ambayo ni Hospitali ya Taifa.

Aidha, ni vyema pia wadau wanaoshirikiana na serikali kwenye kupambana na corona wakasaidia pia kufikisha maji maeneo mbalimbali ambayo hayana huduma hiyo hasa kwenye masoko ya halmashauri, miji , majiji na miji midogo ili kuhakikisha kuwa wananchi wananawa kikamilifu.

Tunatoa wito kuwa ni vyema pia kampuni wahisani zikasaidia kuwafikishia maji wakazi wa maeneo mbalimbali ya mijini ambao hawana maji. Ni vyema pia kuwatafuta na kuwasaidia wahitaji. Wengi wa familia masikini tunaamini taarifa zao zipo kama ambavyo walikuwa wanahudumiwa kupitia mradi wa TASAF.

Tunawasihi wahisani hao waone uwezekano wa kuwafikishia maji familia zenye wahitaji zikiwamo za wajane , yatima na wazee ambao hawana uwezo wa kufikiwa na huduma hiyo, ikizingatiwa kuwa maji ni bidhaa ghali kwa maeneo mengi nchini na ni huduma ghali mno kwa wahitaji.

Tunaona kuwa katika kipindi hiki pamoja na kuunga mkono serikali kwa kuipatia fedha na vifaa , ni vyema pia kuwakumbuka walio na shida ya maji hasa wahitaji ambao wengi ni wanawake na watoto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Sababu hizi za mimba kwa wanafunzi zitaisha lini?

Na Sabato Kasika

**TAMAA** ya kutaka kupata mali, ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi, umbali wa shule na hasa sekondari za kata, ni miongoni mwa sababu zinazotajwa kuchangia mimba kwa wanafunzi.

Hizo ndizo sababu zinazotajwa kila mara, licha ya kuwapo juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kukomesha tatizo hilo linalokatiza ndoto za watoto wa kike.

Kwa ujumla ni kwamba, mimba bado zimeendelea kuwa sababu zinazochangia kuwapo tatizo hilo, hivyo kuna haja ya kutafakari na kuchukua hatua zaidi kwa ajili ya ufumbuzi wa kudumu.

Nikianza na mabweni, yawezekana kweli yakawa na mchango katika kuwapunguzia wanafunzi vishawishi, ambavyo wanakutana navyo njiani ikiwamo lifti za bodaboda wanapotembea umbali mrefu.

Inawezekana mwanafunzi akakataa lifti, lakini akibembelezwa, mwishowe anaona labda dereva wa bodaboda ana nia ya kweli ya kumsaidia na kumbe ndiyo anajiingiza katika mdomo wa mamba.

Hivyo, kwenye ujenzi wa mabweni, ni vyema sasa jamii ishiriki kikamilifu katika kufanikisha ujenzi huo ili kupunguza kama siyo kumaliza tatizo hilo linalosababisha kupata mimba.

Ikumbukwe kuwa, hata wale ambao hupanga vyumba mitaani kutokana na ukosefu wa mabweni, bado wako kwenye hatari kubwa ya kukumbana na vishawishi vinavyoishia mtegoni.

Jamii ikikaa pembeni kwenye suala hilo la kujenga mabweni na kujiona haihusiki, itakuwa vigumu kumaliza tatizo la mimba kwa wanafunzi, kwa hiyo ushiriki wa jamii hata kwa kutoa nguvukazi ni muhimu.

Kwenye suala la elimu ya afya ya uzazi, kila mzazi ana jukumu la kumfundisha mtoto wake kujitambua kadri anavyokua ili hatimaye aweze kukabiliana na changamoto zilizo mbele yake.

Lakini, bahati mbaya wazazi wa zama za sasa wako 'bize' kuhangaikia maisha na kuwaacha watoto wakijilea wenyewe. Matokeo yake, wanajikuta kwenye vishawishi wanavyoshindwa kukabiliana navyo.

Wanapokwama kukabili vishawishi, wanaweza kujikuta wanaangukia katika uhusiano usiofaa na kupata mimba zisizotarajiwa na kulazimika kukatisha masomo.

Vilevile, kuna suala la umaskini wa kipato kwenye baadhi ya familia, nalo linatajwa kusababisha mimba, kutokana na baadhi ya wazazi kuwa na tamaa ya kupata mali na wanawageuza mabinti zao kuwa mitaji.

Hili nalo wakati mwingine linaambatana na utamaduni wa baadhi ya makabila nchini, ambayo ni jambo la kawaida mtoto wa kike kupata mimba kukubali kupewa chochote na mharibifu ili mambo yaishe kimyakimya.

Mtu akichukua muda wa kutafakari sababu zinazoendelea kuchangia kuwapo kwa tatizo la mimba, atabaini kuwa ziko ndani ya uwezo wa jamii, haijaamua kubadilika na kuchukua hatua.

Ni kweli wapo baadhi ya watoto wa kike walioshindikana, lakini ukubwa wa tatizo la mimba usingekuwa wa kiasi hicho, ambacho kimekuwa kikitajwa kama kila mmoja angetimiza wajibu wake.

Kwa mfano, wanafunzi 184 kati ya 2,091 wa shule za msingi na sekondari mkoani Pwani, wamekatisha masomo kutokana na kupata mimba kwa mwaka 2019, huku shule za msingi ni 40 na 144 wa sekondari.

Ni taarifa ya Ofisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Abdul Maulid, aliyowahi kuitoa kwenye kikao cha wadau wa elimu, akisema utoro nao ni moja ya vikwazo katika suala la elimu mkoani humo.

Suala la umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shule, nalo linatajwa kuwa kikwazo kwa wanafunzi, pia kutokuwapo kwa chakula cha mchana shuleni, nako ni tatizo lingine.

Lakini, kimsingi vyote hivi ni kama viko ndani ya uwezo wa jamii, hivyo kuna haja ya kutafakari na kisha kuchukua hatua za kushiriki kikamilifu katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

Ikumbukwe kuwa shule za msingi na sekondari za serikali ni mali ya umma na umma ni jamii yenyewe, hivyo una wajibu wa kuzihudumia ikiwamo kujenga mabweni, miundombinu mingine na chakula.

Hayo yakifanyika, itakuwa ni rahisi kukazania masomo ya watoto na kuweka kando dhana ya kuwaozesha au kuendekeza mahari kutoka kwa wanaowapa mimba, hali inayovurugia ndoto za baadaye katika taaluma.

HABARI KITAIFA

## Adakwa tuhuma wizi fedha kwa mtandao

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

MKAZI wa Mtoni kwa Azizi Ali, jijini Dar es Salaam, Grace Rauwo (31), anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma, kwa kosa la wizi kwa njia ya mtandao.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa na gari namba T 745 DSS aina ya Toyota Crown, ambalo analitumia katika uhalifu, na linadhaniwa kuwa ni la wizi.

"Huyu anafanya uhalifu huu na timu ya wenzake wakiwa wanajihusisha na wizi wa fedha kwa njia ya mtandao wakiwa wamejisajili kama mawakala, hawa wamechonga laini za simu wanaingilia mifumo ya neno siri za wateja na kuiba fedha," alisema Muroto.

Alisema kabla ya kukamatwa walikuwa wameiba fedha kwa njia ya mtandao Sh. milioni 27 na kugawana, huku yeye akiamua kununua gari hilo.

Wakati huo huo, Muroto alisema Polisi wamebaini kuwa magari yanayoibiwa mkoani Dodoma ni yale yanayotumia funguo za 'Sensor' ambazo hazihitaji kuchongwa.

"Tunawashauri kuchukua tahadhari zote ikibidi wafunge 'Car truck system' kwenye magari au CCTV kamera kuongeza utambuzi wa wahalifu baada ya matukio," alisisitiza.

Aliwataka wenye magari kuchukua tahadhari kuhifadhi magari yao katika mazingira salama ikiwamo kuepuka kuegesha magari kwenye mazingira yanayowavutia wahalifu kuiba.

"Pia chukueni tahadhari wenye magari kuwa makini na waosha magari, mafundi, madereva wanaotumia kusafirisha au kusafiri nao safari za mbali," alisema.

# Familia ya kijana aliyeuawa Dar kwenda mahakamani

**Na Enock Charles**

FAMILIA ya kijana Claud Manda (20), imesema itakwenda mahakamani kutafuta haki ya mtoto wao anayedaiwa kushushiwa kipigo na polisi kilichosababisha kifo chake.

Akizungumza na gazeti hili wakati wa mazishi yaliyofanyika jana Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mama mzazi wa kijana huyo, Subira Rashid, alisema hawatakubali na kilichofanyika bali watakwenda mahakamani kuitafuta haki.

"Kwa kweli mwanangu siwezi kukubaliana na hali hii, nitaenda mahakamani kuitafuta haki ya mwanangu Claud haikuwa vyema kumpiga hadi kumuua hata kama alikuwa na makosa," alisema.

Kijana huyo inadaiwa kuwa alikamatwa na wenzie sita eneo la Kinondoni Moscow na polisi na kisha kupigwa na kufikishwa katika kituo cha polisi cha Hananasif na baadae kituo cha Oysterbay, vyote vya jijini Dar es Salaam, wakiwa katika hali mbaya na alipozidiwa polisi walimpeleka Hospitali ya Mwananyamala, hata hivyo juhudi za matibabu zilishindwa kuokoa maisha yake.

Babu wa marehemu, Lucas Manda akizungumza na gazeti hili katika Hospitali ya Mwananyamala Jumatatu wiki hii, alieleza kusikitishwa na tukio hilo la mjukuu wake kupigwa hadi kufariki dunia huku wenzie saba wakidaiwa kuendelea kushikiliwa polisi. "Wale vijana walikutwa ndani, wanavyodai ni kwamba walikuwa wanavuta bangi hawajakuwa na makundi mabovu wala nini ni bangi tu wanavuta, sasa katika kuvuta unajua ni vijana katika vijiwe vyao sasa wale jamaa wakaingia mule ndani wakaanza kuwapiga mikong'oto wakaburuzwa mpaka kituo cha polisi," alieleza Manda.

Akimuelezea marehemu huyo, mmoja wa marafiki zake ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini alisema marehemu huyo alikuwa akijishughulisha na shughuli za ujenzi na alikuwa na bidii ya kazi huku akiheshimu watu wa rika zote. "Claud alikuwa poa sana alikuwa na bidii na nidhamu kwa kila mtu uwe mdogo au mkubwa," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Edward Bukombe, akizungumza na Nipashe baada ya kutokea taarifa za tukio hilo, alithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao akiwamo marehemu kwa makosa mbalimbali, lakini hafahamu kama kuna mmoja ameuawa na polisi na kwamba ukweli wa jambo hilo utafahamika baada ya polisi kufanya uchunguzi.




Dereva wa bajaji akiwa amepakia mzigo wa magodoro juu mjini Iringa jana, kitendo ambacho ni kinyume na sheria za usalama barabarani. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mkurugenzi kortini kwa madai uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Salsabil Investment Limited, Abdulrahman Omary, amefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na kesi ya Uhujumu Uchumi yakiwamo mashtaka 15, kuratibu genge la uhalifu, kusafirisha mazao ya misitu yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 452.7.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, alidai kati ya Januari mosi na Novemba 31, 2015, mahali tofauti, aliratibu genge la uhalifu. Komanya alidai kuwa tarehe za tukio la kwanza kati ya shtaka la tatu mpaka la 14, mshtakiwa alighushi nyaraka za kusafirisha mazao ya misitu aina ya magogo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alighushi nyaraka ya kusafirisha mazao ya misitu kontena 17 akidanganya kuwa kibali hicho kimetolewa na ofisa mwenye dhamana nchini Zambia wakati akijua si kweli.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe isiyojulikana kwa lengo la kudanganya alitoa nyaraka ya uongo ikiwamo kibali cha kusafirisha mazao ya misitu katika ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), akionyesha nyaraka hiyo imetolewa na ofisa mwenye dhamana nchini Zambia wakati akijua si kweli.

Komanya alidai katika shtaka la ukwepaji kati ya Januari mosi na Novemba 31, 2015 jijini Dar es Salaam kwa nia ya kukwepa kulipa kodi alitoa nyaraka ya uongo yenye thamani ya Sh. 452,787,676 kwa TRA wakati akijua kufanya hivyo ni kosa.

Katika shtaka la kutakatisha fedha, mshtakiwa anadaiwa kujipatia fedha hizo kama zao la kosa tangulizi la kukwepa kodi.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Komanya alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 22, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (wa pili kulia), akikabidhi barua na kitambulisho kwa Balozi wa shina namba 2 la CCM Kivukoni, Grace Francis, ofisini kwake, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri abaini kiwanda kwenye makazi

**Na Mwandishi Wetu,**
BAGAMOYO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, katika ziara ya kushtukiza, amejiridhisha yeye na ujumbe wake Kwamba, kiwanda cha Axel Chemical kimejengwa katika makazi ya watu katika eneo la Zinga, Wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Aidha, ujumbe umegundua kwamba, kiwanda kinatengeneza bidhaa na kuzifungasha kwa jina tofuuti na lile ambalo limesajiliwa serikalini.

Akizungumza kwa njia ya simu kutoka India, mmiliki wa kampuni hiyo, Prashant Detha, alikiri makosa aliyoelezwa na Waziri Zungu na hasa la kufungasha bidhaa katika mifuko yenye jina tofauti na lile lililomo katika nyaraka za usajili serikalini.

"Makosa yote tutayarekebisha,"alisikika Detha akimhahidithia waziri.

Hata hivyo, Waziri Zungu aliagiza kiwanda kifungwe mpaka uchunguzi wa kina utakapokamilika juu ya tuhuma dhidi ya uongozi wa kiwanda hicho, uhalali wake, ulipaji kodi na serikali kujiridhisha kwamba mapato yake stahiki yamepatikana.

Waziri alisema kitendo cha kampuni hiyo kuzifungasha bidhaa katika mifuko yenye jina tofauti na nyaraka zilizosajiliwa kimekuwa kikiikosesha serikali mapato halali.

"Serikali imekuwa ikipoteza mapato kutokana na udanganyifu unayofanywa na baadhi ya wafanyabishara nchini. Jambo hili linarudisha nyuma maendeleo," alieleza Waziri Zungu na kusisitiza kwamba lazima uchunguzi ufanywe kubaini tuhuma zilizopo ikiwamo kulituhumu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuwa linachelewesha ajenda ya uwekezaji, jambo ambalo alisema siyo la kweli.

"Kazi kubwa inayofanywa na NEMC ni kuhakikisha uwekezaji unafanyika kama azma ya serikali inavyotaka; lakini uwekezaji ufanywe kwa kufata sheria na kanuni ili kulinda mazingira," alieleza Zungu.

Alisema ujumbe wake umebaini mambo kadhaa ikiwamo kiwanda kufanya shughuli za uzalishaji kwa muda mrefu bila cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira, jambo ambalo amsema ni kinyume cha utaratibu na kwamba kiwanda hakitambuliki wilayani japo kimekuwa kikifanya kazi toka 2014. Waziri alisema mamlaka zipo kisheria na ni kwa lengo la kusimamia sheria na kanuni ili kuwe na usawa katika kutekeleza majukumu na kuiletea nchi maendeleo pasipo kuathiri mazingira.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa, aliahidi kwamba wilaya itatoa ushirikiano kwa mamlaka nyingine wakati wa uchunguzi ili hatimaye wilaya ipate kodi stahiki kutoka katika kiwanda hicho.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwaomba wamiliki wa viwanda na wafanyabiashara kufata sheria na kanuni zilizopo ili waweze kufanya biashara kwa amani.

"Rai yangu kwa wafanyabiashara na wenye viwanda kote nchini ni kufuata sheria na kanuni ili wasiingie katika matatizo na vyombo husika kwani sheria haziangalii ukubwa wa mtu wala rasilimali anazomiliki," alisema Dk. Gwamaka.

# Madiwani wamtaka Mkurugenzi kurudisha mil. 15/-

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

MADIWANI katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro wameazimia kuandika barua kwenda Ofisi ya Rais Tamisemi kushinikiza aliyekuwa Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Sudi Mpili, kurejesha fedha za serikali zaidi ya Sh. milioni 15 anazodaiwa kutumia kwa maslahi binafsi.

Uamuzi huo ulifikiwa jana katika kikao cha Baraza la Madiwani Halmashauri wa Morogoro ikiwa ni miaka miwili imepita tangu alipotenguliwa katika nafasi yake baada ya kudaiwa kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Mwenyekiti wa baraza hilo, Kibena Kingu, alisema ni wakati sasa wa kusimamia misingi ya kisheria ikizingatiwa fedha hizo zilitumika katika matumizi binafsi kinyume na taratibu za serikali.

"Kuna maeneo mengine alifanya kama mkurugenzi, lakini kuna maeneo mengine aliomba fedha hizo kwa matumizi yake binafsi kuna vimemo vimeonekana," alisema.

Alisema kufuatia madai hayo, wameamua kumuagiza Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Rehema Bwasi, kumuandikia barua (Katibu Mkuu Tamisemi) ili fedha hizo zirudishwe.

Suala hilo limesababisha Kaimu Katibu Tawala anayeshugulikia Serikali za Mitaa Mkoa wa Morogoro, Christer John, kutolea ufafanuzi kuwa hatua anayopaswa kuchukuliwa ni kufuata utaratibu kuanzia ngazi ya mkoa.

"Utaratibu unaopaswa kuchukuliwa kwa sasa ni kumuandikia barua Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro kisha yeye ndio amuandikie barua katibu mkuu wa Tamisemi ili Sudi Mpili arudishwe hapa," alifafanua.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Rehema Bwasi, alikiri kupokea maelekezo hayo kutoka kwa Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani na kusema kuwa hatua zitachukuliwa ndani ya kipindi kifupi.

"Nimepokea maelekezo yenu, msimamo wa halmashauri ni kuendeleza ushirikiano katika kufanikisha usimamizi wa shughuli za serikali ikiwamo usimamizi wa miradi ya maendeleo na matumizi bora ya fedha za umma," alisema mkurugenzi.

Katika kikao hicho cha robo ya pili ya mwaka huu wa fedha iliwasilishwa pia taarifa ya Mkaguzi wa ndani, pamoja na mambo mengine taarifa hiyo ilisisitiza kuzingatiwa kwa taratibu za kisheria hasa katika mfumo wa udhibiti wa manunuzi pamoja na hati za malipo.

# Takukuru yashtukia fedha za uchaguzi rushwa majimboni

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeonya wanasiasa wanajipitisha kwenye majimbo mbalimbali huku wakitoa rushwa kwa ajili ya kushawishi kupata nafasi ya kuongoza.

Aidha, pia wamewaonya wananchi wanaojihusisha na rushwa hizo kuwa hatua zitachukuliwa dhidi yao kwa kuwa ni kosa kisheria kutoa na kupokea rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia John Mbungo, alisema kuna viashiria vya vitendo vya rushwa katika baadhi ya majimbo nchini na kwamba taarifa zimeifikia taasisi hiyo.

Aliwataka wananchi kujiepusha na rushwa hizo za wagombea nafasi za uongozi na kutoa taarifa kwa taasisi hiyo wanapoona viashiria hivyo.

"Yapo mambo yasiyoeleweka ambayo yameanza kujitokeza majimboni, na taarifa zake kubainishwa na takukuru" alisema Brigedia Mbungo.

"Takukuru inakemea harakati zote zinazofanyika mapema kabla ya kipenga cha kuanza kampeni kupulizwa," alisisitiza.

Pia alionya watumishi wa Serikali kuingia katika shughuli za kisiasa kwa lengo la kutaka kuchaguliwa wakiwa bado ni watumishi kutambua kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Alisema sheria imeeleza kuwa kama mtumishi anataka kuingia katika siasa basi ni vyema akaachana na utumishi wa Serikali kwanza.

Kuhusu matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo, alisema upo utaratibu ulioainishwa kwa sheria ya kusimamia mfuko wa kuhamasisha maendeleo ya jimbo ya mwaka 2009 na si kutumia vinginevyo.

Aidha, alionya matumizi ya fedha binafsi za wabunge ili wasiingie katika mtego wa rushwa kwa kuwa ipo sheria ya kudhibiti gharama za fedha za uchaguzi ya mwaka 2010 itakayosimamia suala hilo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 taasisi hiyo ilifanikiwa kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 82.8 ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.7 kutoka kiasi cha Sh. bilioni 70.3 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Alisema miradi ya maendeleo iliyofanyiwa ufuatiliaji nayo ikiongezeka kutoka 691 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.494 hadi miradi 1,106 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.668.

## HABARI KITAIFA

# Wasionawa mikono mnadani faini 50,000/-

**Na Gurian Adolf,** NKASI

ILI kukabiliana na kuenea kwa maambukizi ya homa kali ya mapafu corona inayosababishwa na kirusi cha COVID-19, uongozi wa Wilaya ya Nkasi umetangaza kuwa watakaobainika wameingia eneo la mnada bila kunawa mikono watatozwa faini ya Sh. 50,000.

Adhabu hiyo pia itawahusu wafanyabiashara watakaokaidi kuweka maji tiririka na sabuni ya kunawia mikono kwa wateja wao katika maeneo wanayofanyia biashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Missana Kwangula, aliyesema hayo wakati akizungumza na Nipashe, na kusema katika mnada uliopita, watu kumi walitozwa faini ya Sh. 50,000 kwa kuingia eneo la mnada bila kunawa mikono, hivyo kuiingizia halmashauri yake mapato ya Sh. 500,000.

Alisema maeneo ya minada yatakuwa na uzio, ambapo miti itasimikwa na kuzungushiwa kamba ya katani ili watu wasiingie bila kunawa mikono.

Aliongeza kuwa kutakuwa na milango miwili ya kuingia na kutokea, huku kukiwa na tenki kubwa la maji ya kunawa mikono, sabuni na vitakasa mikono, na kwamba wafanyabiashara wakiwamo mamalishe watahamasishwa kuwa na ndoo za maji na sabuni katika maeneo yao ya biashara.

'Ili kubaini kuwa wamenawa mikono yao, kila mwananchi kabla ya kuingia eneo la mnada akishanawa mikono yake basi anachovya kidole cha mwisho cha mkono wake wa kushoto kwenye kidau cha wino kama vile amepiga kura," alisema na kuongeza:

"Baada ya muda ukaguzi utaanza kwa kila mmoja kuonyesha kidole chake kama kina alama ya wino. Mnada uliopita tuliwakamata kumi kila mmoja wao alilipa faini ya Sh. 50,000 tukakusanya kiadi cha Sh 500,000 pamoja na makusanyo mengine tukafikisha Sh. 7,500,000."

"Maofisa wa afya watapita kila nyumba ya biashara kukagua na mfanyabiashara atakayebainika hajaweka maji na sabuni ya kunawa wateja wake, atatozwa faini ya Sh. 50,000.

Maria Adam, mfanyabiashara ya duka katika Mji Mdogo wa Namanyere, alisema bei ya ndoo ya maji yenye ujazo wa lita 20 awali ilikuwa ikiuzwa Sh. 10,000, lakini sasa bei imepanda na zinauzwa mpaka Sh. 25,000.

"Hapa ndoo hizi zimeadimika, zinaletwa na wafanyabiashara kutoka Mbeya, licha ya bei kuwa kubwa, tumezinunua hivyo hivyo," alieleza John Chiwalala




Wachuuzi wa mboga, wakizipanga vizuri kwenye mabeseni kwa ajili ya kuwavutia wateja katika eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watumishi, CCM wadaiwa kulipa kiduchu halmashauri

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kupitia upya gharama za vibanda vya biashara vilivyopo katika mji huo ili bei ziendane na uhalisia kwa kuongeza mapato.

Aidha, amedai zipo taarifa kuwa waliopangishwa ni watumishi wa halmashauri na wana-CCM, na ndiyo wanaozuia kodi halisi kutozwa kwenye vibanda hivyo.

Alisema watu hao hulipa Sh. 5,000 kwa mwezi kwa halmashauri huku wao wakivipangisha kwa Sh. 80,000 hadi 100,000 jambo ambalo siyo sahihi.

Akizungumza na viongozi, watendaji, watalaamu na kamati ya fedha wa Halmashauri ya wilaya hiyo katika mji mdogo wa Nachingwea, alisema uhalisia huo utasaidia kuongeza mapato na kwamba kinachoendelea ni udanganyifu

Mkuu huyo wa mkoa alikuwa kwenye ziara kukagua vituo maalum vya kupokea watakaobainika kuwa na corona, ndipo alipokutana na wataalam wa kamati ya fedha kupata maelezo jinsi halmashauri ilivyojipanga.

Kwa mujibu wa Zambi, haiwezekani katika hali ya sasa banda moja la biashara likapangishwa kwa Sh. 5,000 kwa mwezi, kwa kuwa uhalisia ni wahusika wanapokea fedha kutoka kwa waliowapangisha na wao hawafanyi biashara humo.

Aidha, alisema yawezekana baadhi ya waliopangishwa kwenye vibanda hivyo ni watumishi wa Halmashauri, viongozi katika CCM na Madiwani ndiyo sababu jambo hilo limekuwa gumu.

Akipokea agizo hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nachingwea, Hassani Rugwa, alimueleza Mkuu huyo kuwa amelifanyia kazi suala hilo, na kwamba vibanda vilivyopo kituo cha mabasi vilijengwa na wafanyabiashara wenyewe, baada ya kutakiwa wavijenge ili liwe eneo la biashara.

Pia, alisema licha ya kuruhusiwa, lakini kiwanja hicho ni mali ya Halmashauri, jambo linaloleta utata pale wanapotaka kuzungumzia kuhusu vibanda husika kama ni mali ya Halmashauri au ya wafanya biashara waliotumia gharama zao kuvijenga.

Alisema kwa kushirikiana na Mwanasheria wa Halmashauri hiyo, waliamua kufualitia hati miliki ya eneo hilo, ili kujiridhisha kuhusu uhalali wa umiliki wa mahali hapo na kuwaita wanaoshikilia vibanda hivyo ili kwa pamoja waweze kujadili jambo hilo hata hivyo wafanyabiashara waliofika kwenye mkutano huo walikuwa watatu tu. Mkurugenzi huyo alisema kufuatia hali hiyo, ameitisha kikao kingine na iwapo hawatatokea tena, uongozi wa halmashauri utapanga na kutangaza bei ya pango, ambayo kila anayemiliki kibanda atapaswa kulipa kwa kuwa tangu walipojenga vibanda hivyo na kuvifanyia biashara, walisharejesha gharama zao.

# CT-Scan Muhimbili yaharibika, yaagizwa Ujerumani

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema tayari imeagiza kifaa cha kutoa mionzi ya kupiga picha kwenye mashine ya CT-Scan, kilichoharibika Aprili 7, mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma wa Muhimbili, Aminiel Aligaesha, alilieleza Nipashe alipoulizwa kuhusu habari zilizokuwa zinasambaa kwenye mitandao ya kijamii kuwa CT-Scan ya hospitali hiyo kuu ya taifa haifanyi kazi.

Alisema kifaa hicho wameagiza kutoka nchini Ujerumani na kwamba watafahamu kama kitaingia lini katika siku chache zijazo.

"Ni kweli mashine hiyo haifanyi kazi kuanzia mchana wa Aprili 7, mwaka huu baada ya kuharibika kifaa kinachotoa mionzi ya kupiga picha(CT-Sca X-Ray Tube). Tayari tumeagiza nchini Ujerumani," alisema Aligaesha.

Alisema kuwa wagonjwa wa dharura wanaohitaji huduma hiyo wanawapeleka Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) na wengine wanawahudumia katika hospitali ya Mloganzila.

CT-Scan hiyo, ilinunuliwa na Serikali Januari mwaka 2016, baada ya agizo la Rais John Magufuli alilolitoa, akiutaka uongozi wa MNH kuboresha huduma zake kwa kuhakikisha vifaa tiba na dawa vinapatikana ili Watanzania wapate huduma bora ya matibabu.

Mashine hiyo ilikuwa ya kwanza kuwapo nchini na kwa wakati huo katika nchi za Afrika Mashariki, hospitali iliyokuwa na mashine kama hiyo ni Aga Khan ya nchini Kenya.

CT-Scan (Computerized Tomography Scan) ni aina ya kipimo cha kuchunguza tishu na ogani za mwili kwa kutumia mionzi ya X-ray.

Mashine ya CT-scan kwa sasa zinapatikana katika hospitali za rufaa nchini na huweza kupima sehemu zote za mwili, kuanzia kichwani mpaka miguuni.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angellah Kairuki, katika kikao cha Bunge, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Serikali yafafanua wanaopaswa kupewa chanjo cha Hepatitis B

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema siyo wananchi wote wanapaswa kupata chanjo ya Hepatitis B, bali ni wale walio katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya homa ya ini.

Aidha, utaratibu wa utoaji chanjo utafanyika kwa awamu, kwa kuanzia kwenye hospitali za rufani za mikoa na baadaye kwenye hospitali za halmashauri na utatolewa kwa kuchangia gharama.

Wizara hiyo ilitoa majibu hayo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kutoa chanjo ya Hepatitis B kwa Watanzania ambao hawajapata chanjo.

Kwa mujibu wa majibu ya Wizara hiyo, utaratibu huu utafanyika kwa awamu kwenye hospitali hizo ili wananchi wenye uhitaji na watapata chanjo kwa kuchangia gharama kwa kiwango kitakachowekwa na Serikali.

Awali, ilisema serikali imekuwa ikitoa chanjo ya Hepatitis B kwa watoto wote kupitia chanjo ya Pentavalent yenye mchanganyiko wa chanjo za dondakoo, kifaduro, pepopunda, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo (DPT-HepB-Hib) kuanzia mwaka 2002, hivyo kuhakikisha kuwa wananchi wote waliopata chanjo hiyo wakiwa wachanga.

"Kwa wananchi wengine ambao wamezaliwa kabla ya mwaka 2002 na hivyo kutokupata chanjo hii, Serikali imekwishaainisha makundi maalum ambayo yatapatiwa chanjo kwa kuchangia gharama,"ilisema.

Ilitaja makundi hayo kuwa ni watu ambao kazi zao zinawaweka katika hatari zaidi ya maambukizi, na ni watumishi wa afya wanaohudumia wagonjwa, wanaofanya upimaji katika maabara.

Wengine ni wanaohudumia kwenye vyumba vya maiti, wanaotoa huduma za uzazi na upasuaji, wanafunzi wanaofanya mazoezi ya vitendo kwenye hospitali wakiwa mafunzoni na wafanyakazi wengine ambao huwa karibu na damu au majimaji kutoka mwilini mwa binadamu kutokana na shughuli wanazofanya.

"Kama wanaochangia damu, watumiaji sindano wa madawa ya kulevya, wale wanaoshi karibu na wagonjwa au wanao wauguza wagonjwa wa homa ya ini, wafungwa na watu wenye wapenzi wengi, watu ambao hali yao ya ugonjwa inawaweka katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya Homa ya Ini mfano walio kwenye "haemodialysis" au walio na maambukizi ya VVU au magonjwa ya TB, kisukari," ilisema.

Kadhalika, ilisema wengine ni wasafiri wanaokwenda kwenye maeneo yaliyo na kiwango kikubwa cha maambukizi ya Hepatitis B au kwa matakwa ya nchi husika, na kwa maombi ya mchanjwaji na madereva na utingo wa safari ndefu.

## Waliopisha umeme Kibaha kulipwa fidia

BUNGE limeelezwa kuwa wakazi wa Kibaha mkoani Pwani, waliopisha ujenzi wa umeme wa msongo wa Kilovoti 400, watalipwa fidia baada ya serikali kukamilisha taratibu za malipo yao.

Kauli hiyo ilielezwa bungeni jana na Wizara ya Nishati ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Mary Muro.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema serikali ilishafanya uhakiki kwa wakazi wa Kibaha waliopisha ujenzi wa umeme wa msongo wa KV 400.

"Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema hadi kufikia Machi, 2020, taratibu zote za uandaaji taarifa na majedwali ya fidia zilikamilika.

Ilisema jumla ya fidia kwa ajili ya maeneo kati ya Kiluvya (Kisarawe) hadi Chalinze ni Sh. bilioni 21.569 na malipo hayo yanahusisha wakazi watakaopitiwa na mradi katika halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Chalinze.

"Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imekamilisha taarifa ya uhakiki wa wananchi wote wanaostahili kulipwa fidia ya mali zao, kinachofanyika kwa sasa ni kukamilisha taratibu za malipo kwa wananchi hao," ilisema.

Taarifa ilieleza kuwa serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Dodoma kupitia Chalinze.

Ilisema mradi unahusisha pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Kibaha hadi Zinga Bagamoyo.

"Mradi huu unalenga kuimarisha mfumo wa kusafirisha umeme nchini ikiwa ni pamoja na kusafirisha umeme kutoka mradi wa umeme wa Megawati 2,115 Mwalimu Nyerere (JNHPP)," ilisema.

Pia, ilieleza mradi huo unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa takribani kilometa 600 kutoka Kinyerezi-Chalinze kilometa 100, Chalinze-Rufiji kilometa 160 na Chalinze-Dodoma kilometa 340.

"Mradi unahusisha pia ujenzi wa kilometa 40 njia ya umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Kibaha hadi Zinga Bagamoyo, mradi huu utaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Zinga (Bagamoyo)," ilisema.

Ilibainisha kuwa mwaka 2015 hadi 2016 kazi ya uthamini wa mali za wananchi kutoka Kisarawe, Kibaha hadi Chalinze ilifanyika ili kulipwa fidia na kupisha ujenzi wa mradi.

# Mpango wa kuupatia ruzuku ushirika wa wavuvi wasukwa

SERIKALI imeandaa mpango wa kutoa ruzuku kwa vyama vya ushirika vya msingi vya wavuvi, kutokana na injini za uvuvi hutolewa kwa mfumo wa uchangiaji.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika swali la Mbunge wa Mtambile (CUF), Masoud Abdallah Salim.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema hali ya maisha ya wavuvi nchini katika bahari na maziwa ni mbaya na Serikali kwa mara kadhaa imekuwa ikiahidi kuandaa mkakati wa kuwasaidia vifaa vya uvuvi wavuvi hao wadogo, lakini hakuna utekelezaji.

"Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi hizo?" alihoji mbunge huyo.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema katika ruzuku hiyo, serikali inachangia asilimia 40 na chama cha ushirika cha wavuvi kitatoa asilimia 60 ya gharama ya injini.

"Mpaka sasa jumla ya injini 60 zimechukuliwa na vikundi vya wavuvi 34 vimenufaika na uwapo wa injini hizi," ilisema.

Aidha, ilisema serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya uvuvi nchini kwa kutekeleza mikakati yenye lengo la kuendeleza wavuvi nchini ili kupata ajira, lishe, kipato na kuchangia katika pato la Taifa.

Ilisema miongoni mwa mikakati hiyo ni kufuta kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio ili kupunguza gharama za zana na vyombo vya uvuvi.

Hata hivyo, ilisema kwa mujibu wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), injini za uvuvi, malighafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake vinanunuliwa kutoka nchi za Jumuiya hiyo, hupewa punguzo la kodi ama kufutiwa kodi ili kupunguza bei kwa wavuvi.

"Katika kuhakikisha kwamba wavuvi wanakuwa na zana bora na za kisasa, serikali imeendelea kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ili kuwawezesha wavuvi wote kuwa na zana bora na za kisasa," ilisema. Ilimuomba Mbunge huyo kuhimiza wavuvi nchini likiwamo wa jimbo lake kujiunga katika vyama vya ushirika vya msingi ili kunufaika na fursa hiyo.

Kadhalika, ilisema serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kutengeneza boti na zana bora za uvuvi.

"Kwa mfano, viwanda vya kutengeneza boti aina ya "fibre glass" vya Songoro Marine Transport (Mwanza) na kiwanda cha Sam & Anzai Boat Builders na Seahorse East African (Ukanda wa Pwani),"ilisema.

Pia ilisema viwanda vya nyavu kama vile Kiwanda cha Imara Fishnet (Dar es Salaam) na Fanaka Fishnet (Mwanza) vimeanzishwa na vimesaidia wavuvi nchini kupata vyombo na zana bora za uvuvi.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



Ukurasa 13

## Corona ilivyozaa maisha mapya ndani ya biashara



kurasa 12

## Vijana Mwanza walivyowekeza katika sanaa na kuonyesha maana ya ajira

BUFE

Ijumaa Aprili 10, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

BIASHARA

# Tabasamu la Wabunge kwa wazalisha umeme

**Na Gwamaka Alipipi**

UPATIKANAJI umeme wa uhakika nchini ndiyo suluhisho muhimu litakalolisaidia Taifa kufanikisha Sera ya Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, chini ya mkakati wa Rais Dk. John Magufuli.

Katika kufanikisha hilo, ipo mikakati mbalimbali inayofanywa na serikali kuhakikisha Tanzania inakuwa na umeme wa uhakika, ni pamoja na kuanza kwa ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere, katika eneo la mto Rufiji maarufu 'Stieglers Gorge' unaotarajiwa kuzalisha umeme zaidi ya megawati 2,100.

Miaka ya nyuma, tatizo la upatikanaji vifaa vya umeme nchini lilikuwa sugu kwa muda mrefu, hali iliyosababisha Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), kuagiza baadhi ya vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

Hivi sasa asilimia kubwa ya vifaa hivyo vya usambazaji umeme vinazalishwa nchini, huku baadhi ya viwanda hivyo vinamilikiwa na wazawa kusaidia kuzalisha ajira kwa Watanzania.

Mmojawapo wa wazalisha vifaa hivyo, ni Africab inayozalisha vifaa vya umeme na transfoma kilichopo eneo la Kurasini, jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati, Dustan Kitandula (kushoto kwake), wakipata maelezo kutoka kwa mfanyakazi wa kiwanda cha Africab, David Tarimo. Wa kwanza kulia, ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Mansoor Moiz. **PICHA; MAKTABA**

**ZIARA WABUNGE**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati, ilifanya ziara ya uzalishaji na Mkurugenzi Miuu wa Kiwanda hicho, Mansoor Moiz, aliiambia kuwa wanafanya uzalishaji wa vifaa vyote vinavyotumika katika usambazaji.

Anataja katika baadhi ya maeneo wanakofikisha bidhaa kwenye Mradi ya Umeme Vijijini (REA) nchini na Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco), na bwawa la Mwalimu Nyerere na reli ya kisasa 'Standard gauge.'

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, anaisitiza kwa kauli: "Tayari tumeshapiga marufuku katika uagizaji wa baadhi ya vifaa vya umeme kutoka nje ya nchi, baada ya kujiridhisha na uwezo wa viwanda vyetu vya ndani.

" Vipo baadhi ya vifaa tumeruhusu viingizwe, lakini kadri tunavyoona upatikanaji wake upo wa kutosha hapa nchini, tutasitisha kabisa uingizwaji wake," anasema Naibu Waziri.

Pia, anafafanua kwamba kufanya hivyo, kutasaidia kulinda viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya umeme nchini, hivyo kuviongezea tija na ufanisi katika majukumu waliopewa, kuzalisha umeme majumbani na viwandani.

Anasema ili kulifanikisha hilo, tayari serikali imeunda kamati maalumu kuangalia namna uzalishaji wa vifaa hivyo unavyoweza kutosheleza mahitaji na itakapothibitika kutosheleza, hakutakuwapo sababu ya kuagiza vifaa vya kigeni

Moiz aliieleza Kamati ya Bunge, kwamba kwa sasa kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha kila mwaka nyaya za umeme urefu wa kilomita 75,000, jumla ya transfoma 6,500 na vikombe vya kuunganisha umeme (insulators) 660,000, bomba za plastiki (PVC).

"Kwa sasa hakuna haja ya Tanzania kuagiza tena vifaa kutoka nje ya nchi, kwa kuwa tayari viwanda vya hapa nchini vimeonyesha wazi kukidhi mahitaji ya soko la ndani na hata nje ya soko la Tanzania na zaidi, tunapaswa kuaminiwa," anasema Moiz.

"Katika kipindi cha mwaka huu, tumekusudia kuongeza uwezo zaidi wa uzalishaji wa bidhaa, baada ya kuwekeza katika mashine zenye teknolojia ya uwezo wa juu katika uzalishaji," anatamka Moiz.

Anasema, kiwanda hicho hicho mbali na kusambaza bidhaa zake nchini, pia wana masoko katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Malawi Uganda, Kenya na Zambia, ambako pia wanawekeza kiwanda baada ya kubaini uwepo wa soko zuri.

Wanasema, kuna haja ya kulinda soko la ndani na ushindani wa wamiliki viwanda, haupaswi kuwaumiza wananchi huru watumiaji. Anaziomba mamlaka na ubora, zinapaswa kufanya ukaguzi wa kila mara sokoni

**MWENYEKITI KAMATI**

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dustan Kitandula, anasisitiza umuhimu wa serikali kuhakikisha malipo wanayofanya wakati wa kununua vifaa vya umeme kwenye viwanda hivyo, yawe kwa wakati ili kuwapa nguvu wazalishaji.

Anasema, ili viwanda hivyo vitekeleze majukumu yake ipasavyo, hususani katika wakati uliopo ambao vimepewa jukumu la kuzalisha vifaa kwa ajili ya utekelezaji miradi iliyopo chini ya Rea na Tanesco, malipo yao yaendane na wakati, ili kuwaongezea nguvu ya kufanya uzalishaji zaidi, kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

"Sote tumeshuhudia kazi nzuri inayofanywa na kiwanda hiki na vingine ambavyo tumepata nafasi ya kuvitembelea, vimeonyesha kuwa na uwezo mkubwa katika uzalishaji wa vifaa hivyo na kuondoa ulazima wa uingizwaji vifaa vya umeme kutoka nje ya nchi," anasema Kitandula.

Rai yake kwa uongozi wa kiwanda walichotembelea cha Africab, kuongeza kasi katika uzalishaji, ili kuepuka kuwakwamisha makandarasi katika miradi na anasisitiza kwamba, kwa kufanya hivyo watakuwa wanaenda sawa na sera ya Rais Dk. John Magufuli, kukuza uchumi wa nchi kupitia viwanda.

# Vijana Mwanza walivyowekeza katika sanaa na kuonyesha maana ya ajira

## ■ Walia corona inawaweka njia panda

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

UCHORAJI wa picha za asili na ubunifu wa kutengeneza vitu mbalimbali vya kitamaduni, sanaa, ni ajira tosha na fursa kubwa kwa vijana jijini Mwanza.

Kimsingi, haishii mtu kuajiriwa, iwe msomi au si msomi anaweza kujiajiri, kutokana na shughuli binafsi, badala ya kukaa nyumbani na vyeti akisubri ajira serikalini au kutoka sekta binafsi.

Mfano hai uko jijini Mwanza, ambako kuna waliojiajiri uchoraji picha za asili na ubunifu wa kutengeneza sanaa mbalimbali vya kiutamaduni, wakipatikana katika Mtaa wa Kapripointi.

Wanasema, waliamua kuungana kuanzisha chama kitwacho, Kapripoint Alt Group, kilichoanza rasmi mwaka jana, wakifanya kazi za kisanaa, ufumaji, uchoraji, ushonaji wa mavazi ya kiutamaduni ya aina tofautii.

**MWENYEKITI**

Mwenyekiti wa chama hicho, Mohamed Mwilola, anaiambia Nipashe kuwa, kazi yake ni kufuma vikapu, bangili za asili mkononi na vitambaa mezani, vilevile anashona nguo za kiume na kike, zikiwamo za watoto kwa maana ya suruali, mashati, gauni, kofia, batiki na vikoi.

Anasema, ni ujuzi uliomuajiri na wateja wake wakubwa wanatoka Italia na wachache nchi zingine, ingawa sasa wamekwamishwa na kuwapo maradhi ya corona.

Mwilola anasema, watalii wanapoenda katika Hifadhi ya Taifa ya Sanane na Mbuga ya Serengeti, hufika hapo kununua bidhaa zao, zinazojumuishwa na picha mbalimbali za wanyama kama simba, twiga, kiboko, watu, ndege na vitu vya kisanaa, wakiziuza kwa bei ya Sh. 200,000 hadi Sh. milioni moja.

**UCHORAJI**

Martin Amos (25), mchoraji wa picha za asili na mbunifu wa kutengeneza vitu mbalimbali vya kitamaduni na sanaa, anajivunia uchoraji unatosha kumuajiri, huku akiwa na nasaha kwa msomi na asiye msomi kutosubiri kuajiriwa.

Kijana huyo ni mtaalamu wa kuchora picha za asili na anatengeneza vitu mbalimbali vya kiutamaduni, sanaa na kandambili za Kimasai, akitumia ngozi ya ng'ombe.

Anasema, ni kazi aliyoanza tangu masomoni, katika Shule ya msingi Mlimani, jijini Mwanza, darasa la nne mwaka 2005 na sababu alipenda sana fani hiyo, hata kila alipotoka shule alihamia katika kujifunza hilo.

Baada ya darasa la saba na kuendelea sekondari hadi mwaka 2012 alipohitimu, ndipo alipoamua rasmi kujiajiri katika fani hiyo na kwa sasa anachora picha za wanyama kama tembo, nyati, twiga nyumbu, chui, simba, swala, pala, sambamba na nyumba na watu.

"Vilevile kazi zingine tunazozifanya na wenzangu,ni kuuza nguo za kitamaduni kama vile, vikoi, shuka za kimasai, tisheti (fulana),shati, vinyago,viatu vya kike na kiume, mapambo ya ndani na nje, vitu vya udongo, urembo wa mikononi na shingoni, shanga na heleni, vinavyotengenezwa katika mikoa ya Tanga na Mtwara.

Malengo yake ya baadaye, ni kupanua mtaji awekeze biashara ya duka kubwa la bidhaa za kitamaduni na vitu vya sanaa zikiwamo picha anazochora, kisha anajikita katika kilimo na ufugaji.

Anataja fursa zake za masoko ni kwa watalii wa nchi za Marekani, Denmark, Ufaransa na Ujerumani, wanaofika nchini kutalii kwenye Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Sanane na Mbuga ya Wanyama Serengeti.

"Kuanzia miezi ya Mei watalii wengi huja hapa nchini na kufika jiji la Mwanza kwa ajili ya kwenda kufanya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Sanane, ndipo hapo na sisi hupata neema kubwa na fursa ya kuuza biashara zetu za picha tunazochora za asili na vitu mbalimbali vya kitamaduni na sanaa, wanavipenda sana," Amos anasema.

Anasema vivutio hivyo vya kitalii vimewasaidia kupata fursa, ambayo sasa imevurugwa na janga la corona, serikali imezuia wateja wa nje na wa ndani ni wachache sana.

"Picha moja ile kubwa kwa wageni hao wa nje tunauza katika thamani ya fedha za Kitanzania Sh.150,000 hadi Sh.200,000, lakini wakati mwingine tunauza kwa dola ya thamani ya hizo fedha za Kitanzania, wateja wetu wakubwa zaidi kutoka nje ni ujerumani na Marekani, anasema.

"Wateja wa ndani tunawauzia picha ya aina hizo Sh.100,000 hadi 150,000 na wakati mwingine kama wananunua mzigo mkubwa tunawapunguzia bei, kwa sababu ya uzalendo ili kuwavutia waendelee kupenda vitu vya nyumbani kuliko vya kigeni," anasema Amos.

Anasema, hadi sasa watu wa ndani wengi hawafahamu umuhimu wa kazi za mikono na vya kitamaduni

**CHANGAMOTO ZAO**

"Changamoto yetu kwa sasa vijana katika chama chetu ni kutokuwa na soko la pamoja la kuuzia bidhaa zetu, kwa sababu tumesambaa mtaani, lakini kama tungepata eneo tukakaa pamoja hata soko la bidhaa zetu lingekuwa zuri zaidi kuliko sasa," anasema Mwenyekiti Mwilola.

Anataja changamoto nyingine kuwapo janga la corona sasa, linalosababisha wageni wasiingie nchini na biashara zao kusimamisha na imeathiri vipato vyao.

Malengo yake ya baadaye ni kupanua mtaji na kuwekeza biashara ya duka kubwa la bidhaa za kitamaduni, vitu vya sanaa zikiwamo picha anazochora pamoja na kuanzisha kilimo na ufugaji.

**FURSA KIBIASHARA.**

Hata hivyo, fursa nyingi za biashara ya picha na vitu vingine wanaipata kutoka kwa watalii wa nje; Marekani, Denmark, Ufaransa na Ujerumani, wanaokuja nchini kufanya utalii kwenye hifadhi ya taifa ya kisiwa cha sanane na mbuga ya wanyama ya Serengeti.

"Kuanzia miezi ya Mei watalii wengi huja hapa nchini na kufika jiji la Mwanza kwa ajili ya kwenda kufanya utalii katika hifadhi ya taifa ya kisiwa cha sanane, ndipo hapo na sisi hupata neema kubwa na fursa ya kuuza biashara zetu za picha tunazochora za asili na vitu mbalimbali vya kitamaduni na sanaa, wanavipenda sana," Amos, anasema.

Anafafanua kuwapo kwa hifadhi hizo zimesaidia wao kupata fursa ingawa kwa sasa janga la ugonjwa wa corona limeathiri mno biashara zao, kwa sababu watalii kutoka nje ya nchi hawaji tena baada ya serikali kuzuia, lakini wateja wa ndani ni wachache sana wanaoweza kununua bidhaa zao.

"Picha moja ile kubwa kwa wageni hao wa nje tunauza katika thamani ya fedha za Kitanzania Sh.150,000 hadi Sh.200,000, lakini wakati mwingine tunauza kwa Dola(za Marekani) ya thamani ya hizo fedha za Kitanzania, wateja wetu wakubwa zaidi kutoka nje ni Ujerumani na Marekani.

"Lakini wateja wa ndani tunawauzia picha ya aina hizo Sh. 100,000 hadi Sh. 150,000 na wakati mwingine kama wananunua mzigo mkubwa tunawapunguzia bei, kwa sababu ya uzalendo ili kuwavutia waendelee kupenda vitu vya nyumbani kuliko vya kigeni," anasema Amos.

Watu wa ndani walio wengi hawafahamu umuhimu wa kazi ya kutengeneza vitu vya mikono na vya kitamaduni kuwa ni vizuri zaidi kuliko vya kiwandani au vya kigeni kwa sababu, pia vinavutia.

Amos ana rai kwa Watanzania kuwa wanatakiwa kujenga utamaduni wa kusaidia au kupenda vitu vya nyumbani, kuliko vya nje ya nchi, ikiwa ni moja ya kukuza uchumi wa nchi kama vile serikali inavyolenga kufikia huko.

Anaiomba serikali kuendelea kutangaza utalii wa ndani ili wananchi kila mmoja, afahamu fursa zake na faida ya kupenda vitu vyao vya kitamaduni, sanaa na kuwa wabunifu wa mambo mbalimbali ambayo yatakuwa ni moja ya kujiajiri wenyewe hasa vijana na kuanzisha viwanda vidogo, badala ya kutegemea kuajiriwa tu.

- ***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa barua pepe anthonygervas@yahoo.com na namba ya simu: (+255) 0682 869 244, Kanda ya Ziwa.***



Mwenyekiti wa Chama cha Kapripoint Group, Mohamed Mwilola, akiwa katika kazi yake ya kuchora katika banda lake, Mtaa wa Kapripoint jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

> **"Kuanzia miezi ya Mei watalii wengi huja hapa nchini na kufika jiji la Mwanza kwa ajili ya kwenda kufanya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Sanane, ndipo hapo na sisi hupata neema kubwa na fursa ya kuuza biashara zetu za picha tunazochora za asili na vitu mbalimbali vya kitamaduni na sanaa, wanavipenda sana**



Watalii wakifurahia jambo katika kisiwa cha Sanane. Wanapopita jijini Mwanza. Ni wateja wazuri wa bidhaa za sanaa na utamaduni. **PICHA: MTANDAO.**



Waendesha bodaboda wa mjini Moshi. **PICHA: MTANDAO.**

# Ugonjwa wa Corona ulivyozaa maisha mapya ndani ya biashara

## ● Bodaboda, duka jumla, famasia...

**Na Tuntule Swebe**

HIVI sasa corona imeshika kila mahali. Ni sehemu ya maisha ya jamii ilivyo. Biashara nayo haina nafuu hata kidogo.

Wajasiriamali waliohojiwa na Nipashe, nao wana yao ya kujadili kuhusu janga hilo lilivyowakaba ndani ya nyendo zao kimaisha, kutafuta

Katika kujua hayo, Nipashe ilifika eneo linaloitwa Boko Basihaya kupata picha halisi, kiongozi wa mgawaha anayejitabulisha kwa jina la Ericana, mmiliki wa Ericana Café, anasema kwamba tofauti na zamani, hivi sasa wateja wamepungua.

Ericana anasema, ni hali inayompa mtihani katika kipato chake kufikia hatua analazimika kupunguza kipato chake kuwalipa wafanyakazi.

Kwa mujibu wa mmiliki wa mgahawa huyo, imemgharimu zaidi hata katika mapato ya nyumbani, sasa akitafakari changamoto ya ada kwa wanawe, shule zitakapofunguliwa.

Mwendesha pikipiki za abiria, maarufu bodaboda anayejitambulisha kwa jina la Juma Jey, anasema tangu kuzuka kilio cha corona, wateja wa pikipiki wamepungua, watu wakihofu kuambukizwa.

Juma anasema, ni hali inayobadili hata mwelekeo wao wa maisha ya kila siku, hata nyendo za mlo wao kubadilika katika sura ya kubana matumizi.

Mhudumu wa duka la dawa, liliko jirani na stendi eneo la Basihaya, ambaye hakujitaja jina kwa nafasi ya kutetea maslahi ya duka na taaluma yake, pia anasema anaamini watu wengi wanaumwa, lakini wamekwama kimaslahi hata wasifike kununua dawa

Mama huyo anarejea hata nyumbani kwake, kwamba mumewe hadi sasa amesimamishwa kasi kutokana na hali mbaya ya kibiashara iliyoko sasa katika maeneo mengi nchini.

Ni aina ya ufafanuzi ambao, hata sasa Nipashe iligundua kuwa zimetawala katika maduka mbalimbali ya jumla nchini, kwani wateja wamepungua na bidhaa haziuziki kama kasi za zamani.

Pia, ndicho kilichoibua kuwepo kundi kubwa la watoto wanaozurura mitaani bila ya kuwa na kazi maalum za kufanya.

# Tiba corona yaja na vita ya kibiashara mlango wa nyuma

**Na Nimi Mweta**

MIFUMO ya biashara kati ya nchi tofauti duniani na hata ndani ya nchi, imeingia katika majaribu mengine kuhusiana na ugonjwa wa corona.

Ni pale serikali zinapofanya juu chini kupata dawa zinazohitajika kwa haraka, wakati mara nyingi tu zinatoka nchi za nje.

Kwa mfano washauri wa suala hilo katika Ikulu ya Marekani na majopo tofauti yanayofuatilia suala hilo nchini humo, walifikia tamati kuwa dawa ya hydroxylchloroquine inafaa kwa kuanza au kuimarisha tiba ya maambukizi ya corona.Ni dawa inayopatikana nchi za joto na kwenye malaria.

Isitoshe, kitambo tu dawa hiyo ilikuwa imewekewa vizuizi na Shirika la Afya Duniani (WHO) na haikutumika mara nyingi, wakati shirika hilo na serikali nyingi zilipofikia uamuzi wutumia dawa zenye msingi wa kemikali ya salfa (suphur).

Utafiti wake ulikuwa umeharakishwa, kwani nchi nyingi zilitaka kutengeneza dawa zisizokuwa na hatimiliki ya jadi kama klorokwini, hivyo matumizi ya dawa hizo zikiwamo metakefikini na fansida zikaleta madhara tofauti kwa baadhi ya wagonjwa. Mwishowe, WHO iliridhia kutumia mchanganyiko wa 'dawa tatu.'

Nchini Marekani, ubishi umeendelea kuhusu matumizi ya hydroxyl-chroloquine kama dawa ya kutanguliza katika kumhudumia mgonjwa wa corona, ambaye hali yake siyo nzuri.

Wapo wanaoshambuliwa na virusi hivyo, halafu kinga za mwili zinapangua athari za virusi zinapoanza kujionyesha, kwani corona haikai mwilini kama haipati vipokezi asilia, kwa mfano ugonjwa unaokandamiza kinga za mwili kufanya kazi. Corona ikishatulia hapo, hazitafanya kazi tena.

Yako maeneo mapya ya matatizo kuhusiana na tiba zinazofaa na kupatikana dawa husika, kwani sekta ya utengenezaji dawa, ni sehemu ya utandawazi na mara nyingi dawa muhimu au chembe zinazounda michanganyiko ya kutibu magonjwa tofauti inapatikana katika nchi tofauti.

India ni nchi kitovu cha Marekani kuhamishia 'software', yaani uendeshaji wa tafiti nyeti katika mazingira ambayo hayatofautiani sana na Marekani kwenyewe, tofauti na kile inachofanya China, Uwekezaji wake huko ni 'hardware' yaani mitambo; ni nguvu na siyo akili.

Uwekezaji kuhusu ugonjwa wa corona mpya unaendana na juhudi za awali kutafuta dawa na kinga za corona tofauti zilizotangulia, kwa mfano sars inafanana sana na covid-19 na pale mwanzoni corona hii ilikuwa inaitwa Sars mpya.

India ilishaanza majaribio mengi ya dawa za Sars na Mers, aina ya ugonjwa huo iliyojikita zaidi Mashariki ya Kati (hivyo ikaitwa ugonjwa wa kupumua ('respiratory syndrome' ya Mashariki ya Kati).

Hata dawa hii ya hydroxyl-chloroquine, pia inatengenezwa kwa wingi India, kwani kuna malaria kote barani Asia.

Marekani sasa inaihitajii dawa nyingi za hydroxyl-chroloquine na hali hiyo inaleta mgongano kati yake na India, ambayo siyo tu kwamba inahitaji dawa hizo ila kuweka hata akiba.

Isitoshe, dawa hiyo iliacha kutengenezwa maeneo mengi kutokana na ushauri wa WHO, hivyo nchi siyo chache zitakuwa zinataka zipelekwe dawa hizo, kama ilivyo Marekani.

Hata kama hatimiliki ya kuandaa 'formula' ya hydroxyl-chloroquine awali ilitoka Marekani, haina nguvu kwa India kwa suala hili.



Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Marekani sasa inahitaji dawa nyingi za hydroxyl-chroloquine na hali hiyo inaleta mgongano kati yake na India, ambayo siyo tu kwamba inahitaji dawa hizo ila kuweka hata akiba.**

Isitoshe, uhitaji huo wa Marekani kwa bidhaa muhimu inayopatikana India na kwingineko, labda ni kidogo sana au dawa hizo hazijapata uthibitisho wa Shirika la Viwango vya Chakula na Dawa Marekani (Food and Drug Administration) nchini, unaunganishwa na migogoro kadhaa ya kibiashara kati ya nchi hizo mbili.

Mojawapo ni urushaji wa satellite ya India ulioahirishwa katika dakika za mwisho miezi kadhaa iliyopita, ambako mchangiaji mmoja katika twitter alisema Rais Donald Trump wa Marekani, alizuia urushaji dakika 10 tu kabla haujafanyika.

Wanaofahamu jinsi Rais Trump, anavyoendesha masuala ya usalama wa taifa, wanaweza kuelewa kuwa haikuwa ni suala la chuki maalum kuhusu India, kwani amewahi kuzuia hatua nyingine ambazo zisingewapendeza wengi duniani wanauongana na India kwa kulalamikia uzuiaji huo.

Kuna wakati jeshi la Marekani, lilishajiandaa kujibu mapigo kwa mashambulizi nchini Iran baada ya ndege isiyo na rubani (drone, ndegenyuki) kuangushwa na vikosi maalum vya Iran eneo la baharini (la kimataifa, ilivyosema Marekani). Pia alizuia shambulizi Korea Kaskazini.

Ukiangalia unakuta kuna matatizo halisi ya kiusalama wa satellite, ambayo mchangiaji huyo anasema inaweza kuchukua picha nzuri za dunia katika mazingira yoyote ya hali ya hewa.

Ina maana, pia inaweza kuhitajiwa na utawala wa India kuangalia vilipo na vinafanya nini vikosi vya Marekani barani Asia, au meli za kubeba ndege za kivita wakati wowote.

Sasa endapo hakuna uhakika au majadiliano ya awali ya usimamizi wa shughuli za satelaiti hiyo halafu ofisa wa kijeshi wa India avutiwe urafiki na shirika, kampuni au idara ya kijasusi ya China au Russia, swahiba wa miaka mingi wa India licha ya uwekezaji wa Marekani, si Marekani itajihatarisha?

Yako maeneo mengine ya migongano ya kibiashara kati ya Marekani na nchi nyingine ambayo si ajabu yakaathiri hata nchi za ukanda wa kusini mwa Afrika, hasa jumuiya ya SADC, jumuia ya maendeleo inayounganisha ukanda huu.

Tayari mkutano uliofanywa kwa njia ya video wa mawaziri wanaoshughulikia SADC miongoni mwa nchi wanachama umetoa kipaumbele kwa usafirishaji wa vifaa vinavyohitajiwa na nchi wanachama katika kupambana na kuenea wa gonjwa la corona.

Tatizo ni kuwa moja ya nchi zenye uwezo wa kuzalisha vifaa tofauti na hata dawa zinazonakiliwa kutoka nje ni Afrika Kusini na hivi sasa ina mgogoro na Marekani kwa kutayarisha muswada wa sheria kuwa migongano ya hatimiliki au ya kunakili kati ya kampuni za Afrika Kusini na za nje itatatuliwa kwa sheria ya nchini Afrika Kusini.

Marekani imeshaondoa baadhi ya faida za uhusiano wa karibu kiuchumi kati yake na Afrika Kusini na endapo nchi hiyo itazalisha hydroxyl-chloroquine au dawa nyingine ambayo hatimiliki yake ya awali ni Marekani, inaweza kuwekewa vikwazo, na nchi nyingine zikiinunua zijumuishwe pia.



Rais Donald Trump wa Marekani.



# NBS: Corona haijaathiri mfumuko wa bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu(NBS), imesema hadi sasa haijapata athari zozote zitokanazo na ugonjwa wa corona kwenye ukusanyaji wa fahirisi kwa ajili ya kukokotoa mfumuko wa bei.

Aidha, imesema mfumuko huo kwa mwaka unaoishia mwezi Machi, 2020 umepungua kutoka asilimia 3.4 hadi 3.7.

Akitoa taarifa kuhusu mfumuko huo, Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za jamii wa Ofisi hiyo, Ruth Minja, alisema hatua ya kushuka kwa mfumuko inamaanisha kuna kasi ya mabadiliko ya bei ya bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Machi, 2020.

Alisema kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, 2020 kumechangiwa na kupungua kwa bei ya baadhi ya bidhaa za vyakula na baadhi zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia Machi 2020 zikilinganishwa na bei za Machi 2019.

"Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizopungua bei kwa mwezi Machi 2020, zikilinganishwa na bei za mwezi Machi 2019 ni pamoja na unga wa ngano kwa asilimia 2.1, matunda kwa asilimia 5.5, mihogo kwa asilimia 12.9, viazi vitamu kwa asilimia 3.8 na ndizi za kupika kwa asilimia 10.2," alisema.

Alisema baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizopungua bei kwa Machi 2020, zikilinganishwa na bei za Machi 2019 ni pamoja na majiko ya gesi kwa aslimia 2.3, viyoyozi kwa asilimia 1.1, mafuta ya nywele kwa asilimia 2.7 na bidhaa binafsi za mapambo kwa asilimia 2.9.

Hata hivyo, alisema mfumuko huo kwa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Machi 2020, umepungua hadi asilimia 5.3 kutoka asilimia 5.9 kwa mwaka ulioishia mwezi Februari, 2020.

Kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki, Mtakwimu huyo alisema kwa nchi ya Kenya mfumuko umepungua kutoka asilimia 6.06 hadi asilimia 6.37 kwa mwaka ulioishia Februari, 2020.

Aidha, alisema kwa upande wa Uganda mfumuko wa bei kwa kipindi hicho umepungua hadi asilimia tatu kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka ulioishia Februari, 2020.



Sheikh wa mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, akinawa mikono na sabuni kwa ajili ya kujilinda na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, kabla ya kuingia ukumbini kuhudhuria mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA), ngazi ya wilaya, uliofanyika jijini Dodoma jana. Wa (pili kulia) aliyevaa ni Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kampuni yatoa mafuta lita 50,000 kusaidia vita corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI ya Puma Tanzania, imetoa mafuta lita 50,000 ili kuunga mkono jitihada za Serikali za kukabiliana na homa kali ya mapafu (Covid-19) ambapo yatatumika kwenye magari ya kubeba wagonjwa.

Msaada huo umekabidhiwa kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Serikali inayosimamia mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi Mkuu wa Puma, Dominic Dhanah, alisema wametoa mafuta hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100.

"Kipindi hichi Dunia nzima inapambana na ugonjwa wa corona ni wajibu wa taasisi, mashirika na kampuni mbalimbali kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano ya ugonjwa huu," alisema.

Alisema mafuta hayo yatatumika kwenye magari ya kubeba wagonjwa, hospitali na vituo mbalimbali vya afya vinavyoshughulika kuhudumia wahanga wa ugonjwa huo.

"Msaada huu utakuwa katika mfumo wa Card za mafuta za Puma (Puma cards) zipatazo 100 zilizojazwa lita 500 kila moja, Kamati ya Waziri Mkuu itazisambaza card hizi kwa hospitali na vituo vya afya vinavyo pambana na ugonjwa wa Corona kote nchini," alisema.

Hata hivyo, Dhanah alisema Kampuni ya Puma tayari imechukua hatua mbalimbali zinazosaidia kuwakinga wafanyakazi na wateja wake dhidi ya ugonjwa huo ikiwamo kuweka maji yanayotiririka na sabuni katika vituo vyake vyote vya mafuta.

" Pia tunagawa vifaa vingine kwa watendaji wetu vituoni, kwenye matanki ya kuhifadhia mafuta na kwenye viwanja vyote vya ndege , kuweka vitakasa mikono katika ofisi zake zote nchini, kupima joto wafanyakazi na wateja wengine wanaotembelea ofisi za Puma kote nchini," alisema.

Aidha, alisema pia wanatoa elimu kwa umma kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na wataalamu katika kupambana na virusi vya corona.

Alibainisha kuwa Kampuni hiyo inamilikiwa na serikali na Puma Investments Limited, kila moja ikiwa na umiliki wa hisa kwa asilimia 50.

"Kampuni ya Puma ni ya mkondo wa kati kimataifa katika masula ya mafuta na pia kampuni ya mafuta inayojihusisha na uhifadhi mkubwa na usambazaji wa bidhaa za petroli ndani ya Tanzania," alisema.

Alisema kampuni ina uwezo wa kuhifadhi jumla ya lita za mafuta milioni 94 na kuna vituo 56 vya mafuta maeneo mbalimbali nchini na inahudumia viwanja vinane vya ndege.

Waziri Mkuu alishukuru kampuni hiyo na taasisi nyingine kwa misaada ya kusaidia mapambano ya corona, huku akiziomba kampuni, taasisi na mashirika mengine kuiga mfano huo.

# Zabuni huduma biashara miradi kimkakati kimtandao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amesema utoaji fomu kwa ajili ya kufanya biashara kwenye miradi minne ya kimkakati utaanza wiki ijayo kwa njia ya mtandao ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Hatua hiyo imekuja kutokana na kuwapo kwa msongamano wa watu kwenye ofisi za jiji hilo na kumfanya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, kuzuia utoaji wa fomu hizo kwa njia ya kawaida.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kunambi alisema kutokana na uwapo wa ugonjwa huo, wamebadilisha utaratibu wa uchukuaji fomu za kufanya biashara kwenye Soko la Ndugai, Kituo kipya cha mabasi, na eneo la mapumziko Chinangali Park.

Alisema zitatolewa kwa njia ya mtandao kuanzia wiki ijayo, huku akieleza kuwa wakati wanaandaa utaratibu wa uchukuaji wa fomu hizo hawakutarajia kutakuwa na mwitikio mkubwa.

"Wananchi walijitokeza kwa wingi hali iliyosababisha kusitisha utoaji na hivi sasa tumeandaa utaratibu mpya ambao utaondoa msongamano, lakini pia utamuwezesha kila mwananchi aliyeko mkoa wowote nchini kupata fomu bila kusafiri na bila urasimu wowote," alisema.

Alifafanua kuwa, utaratibu huo unatarajiwa kuanza rasmi Aprili 13 mwaka huu na kuwataka wananchi kufuatilia kwenye tovuti ya Jiji la Dodoma.

Kuhusu wananchi ambao tayari wamekwisha chukua fomu Aprili 7, mwaka huu, kwa kutumia utaratibu wa awali, alisema wataingizwa kwenye mfumo moja kwa moja na watatambulika kwasababu tayari ni wateja wao.

"Niwasihi Watanzania waondoe tu dhana ya kwamba kuna watu maalum au wenye fedha ndio watakaofanikiwa kupata nafasi hizo, serikali ya awamu ya tano inaendesha mambo yake kwa uwazi jambo hili halina urasimu," alisema.

Akizungumzia uuzaji wa viwanja, Mkurugenzi huyo alisema Jiji hilo linaendelea na uuzaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali ikiwamo viwanja vya ujenzi wa hoteli, majengo makubwa na viwanda.



HABARI MBEYA

# Maofisa TPA Kyela kuwekwa kitimoto

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameagiza maofisa wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA), kituo cha Kyela mkoani humo, kuitwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ili waeleze sababu ya meli tatu zilizojengwa ndani ya ziwa hilo kutofanya kazi kwa zaidi ya miaka miwili tangu zilipokamilika.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ambayo ilitembelea Bandari ya Kiwira, zilipoegeshwa meli hizo ambazo zimejengwa na serikali kwa zaidi ya Sh. bilioni 21 kupitia Mkandarasi mzawa Kampuni ya Songoro Marine.

Chalamila alisema kitendo cha meli hizo zilizotengenezwa kwa gharama kubwa kuegeshwa kwenye maji kwa muda mrefu bila kufanya kazi ya uzalishaji ni hasara na kwamba ni bora TPA wangeishauri serikali isizitengeneze. Alisema hakuna sababu ya mizigo zikiwamo ndizi zinazozalishwa wilayani Rungwe kusafirishwa kwenda nchi jirani ya Malawi kwa kutumia magari wakati meli hizo zipo na hazifanyi kazi.

"Muda wote nikija hapa nakuta hizi meli zimeegeshwa hapa kwenye maji, sijawahi kukuta zimeondoka, hizi mbili za mizigo zimejengwa kwa Sh. bilioni 5.5 kila moja na hii ya abiria na mizigo imegharimu Sh. bilioni 9.1 na kuna ujenzi mwingine unaendelea sijui wa vitu gani, lakini hakuna mnachozalisha," alisema Chalamila.

Alisema meli hizo hazifanyi kazi kwa sababu watendaji wa TPA sio wabunifu wa kupata mizigo ya kusafirisha na kwamba kuna uwezekano wanawaogopa wamiliki wa usafiri wa barabarani.

Awali, Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abedi Gallius, alisema mpaka kufikia mwezi Machi kwaka huu, walikuwa wamesafirisha mizigo yenye uzito wa tani 1,000 na kwamba wana wateja watatu pekee wanaosafirisha mizigo.

Alisema wateja wawili wapo Mbamba Bay mkoani Ruvuma na mmoja yupo mkoani Mbeya ambaye ni Kiwanda cha Saruji cha Mbeya na wanaendelea na taratibu za kuandaa matangazo ili kuhamasisha wananchi kuzitumia meli hizo.

"Kuna mteja mmoja alikuwa anasafirisha makaa ya mawe, lakini kwa sasa amesimama kutokana na hiki kipindi cha mvua ambacho hakiruhusu watu kuingia migodini, lakini meli ya abiria bado haijaanza kazi na tutaanza na safari za ndani," alisema Gallius.

Aidha alisema mradi wa uboreshaji wa bandari za ziwa hilo umegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ujenzi wa meli tatu, gati na sakafu ngumu.

Alisema ujenzi wa meli mbili za mizigo ulikamilika mwaka 2018 na ya abiria ilikamika mwezi Desemba, mwaka jana, lakini haijakabidhiwa kutokana na vyeti kuchelewa kutolewa na Shirika la Wakala wa Meli nchini (Tasac).

Alisema mradi wa ujenzi wa gati umefikia asilimia 98 na Mkandarasi anaendelea kufanya marekebisho madogo kabla ya kukabidhi na ujenzi wa sakafu ngumu umeshakamilika kwa asilimia 100.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi (kulia), akikabidhi msaada wa nondo kwa viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), jijini Mbeya hivi karibuni, kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya umoja huo unaoendelea katika Kata ya Isyesye. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Usafiri Tazara wasimamishwa kwa siku 5

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

USAFIRI wa abiria na mizigo kwa njia ya treni katika Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara), umesimamishwa kwa siku tano mfululizo baada ya mvua iliyonyesha kwa siku tatu mfululizo katika Bonde la Usangu, wilayani Mbarali kusababisha mafuriko yaliyoharibu miundombinu ya reli hiyo.

Mafuriko hayo yaliharibu miundombinu ya reli hiyo katika eneo la Chimala, wilayani Mbarali umbali wa kilomita 15 kutoka katika stesheni ndogo ya Chimala na kipande kimoja kimesombwa na moja ya madaraja lipo hatarini kusombwa na mafuriko hayo.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo hilo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema kuna hatari ya mvua hiyo kuendelea kuleta madhara kutokana na hali ya utabiri wa hali ya hewa kuonyesha kuwa kuna mvua zaidi.

Alisema chanzo cha miundombinu hiyo kusombwa ni makaravati yaliyowekwa kutokuwa na uwezo wa kuhimili kiwango cha maji yanayopita kipindi hiki cha mvua nyingi.

"Pia inaonyesha kuwa udongo uliotumika kwenye ujenzi wa haya madaraja, sio mzuri kwa sababu umekuwa makazi ya mchwa, wametengeneza mashimo na hivyo kusababisha ubovu huu," alisema Waziri Kamwelwe.

Aliwaagiza wataalamu wa miundombinu hiyo kuongeza matundu kwenye madaraja hayo ili kupunguza maji kujaa upande mmoja wa madaraja kwa maelezo kuwa ndio chanzo cha kuharibika kwa madaraja hayo.

Aliwaagiza maofisa wanaosimamia miundombinu ya reli na barabara kufanya tathimini ya uharibifu wa miundombinu baada ya mvua kuisha ili yafanyike matengenezo makubwa yatakayosaidia kuimarisha miundombinu hiyo.

Alisema baada ya tathmini hiyo, maeneo yote yaliyoathirika yatatengenezwa na kuanza mikakati mipya ya kuimarisha miundombinu hiyo. Alisema serikali kwa sasa inaendelea na mikakati ya kuimarisha usafiri wa treni katika maeneo mbalimbali ili kupunguza uharibifu wa miundombinu ya barabara.

Awali, akitoa taarifa ya uharibifu wa miundombinu hiyo, Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Tazara Mkoa wa Mbeya, Michael Mwachiko, alisema baada ya mvua kunyesha mto Kimani ulifurika katika eneo lote la daraja na kufikia mita nne zaidi kutoka ardhini.

Alisema eneo hilo lina daraja kubwa na makaravati mawili, lakini pia ni eneo ambalo lina mashamba ya wananchi ambao wanalima mpunga kwa kutumia maji yanayopita kwenye makaravati ya Tazara. Alisema baada ya kubaini madhara hayo waliwahi kuanza kazi ya kurekebisha miundombinu hiyo huku wakisitisha shughuli za safari za treni zote za abiria na mizigo mpaka baada ya kukamilisha matengenezo. "Tulifanya kazi kwa siku tano kurekebisha miundombinu hii, tulianza kazi Ijumaa kwa kuanza kujaza mawe hapa na baada ya hapo tukaanza kuirudisha reli kwenye hali yake ndio maana inaonekana hivi ilivyo na operesheni zimerejea," alisema Mwachiko.

Alisema wataendelea kuikagua miundombinu hiyo mara kwa mara ili kuhakikisha uharibifu unaotokea wakati mvua ikiendelea kunyesha unadhibitiwa mapema kuepuka madhara.

Alisema hakuna madhara yoyote ya kibinadamu yaliyotokea kutokana na kuharibika kwa miundombinu hiyo zaidi ya kukwamisha safari za wananchi.

## Tarura yasaini mkataba ujenzi barabara km. 39

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), Mkoa wa Mbeya, imetiliana saini mikataba ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 39 kwa kiwango cha lami katika Wilaya za Mbeya na Rungwe yenye thamani ya Sh. bilioni 16.39.

Mikataba hiyo ilisainiwa jana jijini hapa kati ya Tarura na makandarasi wanne huku zoezi hilo likishuhudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila pamoja na viongozi mbalimbali wa chama na serikali wa wilaya zote mbili.

Akizungumza wakati wa kusaini mikataba hiyo, Meneja wa Tarura Mkoa wa Mbeya, Gerard Matindi, alisema moja ya barabara hizo ni ya mchepuko ya Inyala – Simambwe yenye urefu wa kilomita 16.7 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema kipande hicho kitagharimu Sh. bilioni 7.05 na itapunguza umbali wa magari yanayotoka Rungwe kuzungukia Uyole yanapoelekea Dar es Salaam na maeneo mengine.

"Barabara nyingine ni Masebe - Bugoba – Lutete yenye urefu wa Kilomita 7.2, Masebe – Mpuguso – Bugoba kibaoni yenye urefu wa kilomita 5.0 na Lupeta – Mwiba – Izumbwe zote wilayani Rungwe," alisema Matindi.

Alisema watahakikisha wanasimamia ujenzi wa barabara hizo ili zijengwe kwa viwango vinavyotakiwa na ziendane na kiwango cha fedha zinazotolewa.

Akizungumza wakati wa kusaini mikataba hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwapongeza Tarura kwa kuanzisha miradi hiyo kwa maelezo kuwa itawasaidia wananchi kusafirisha mazao yao kwa urahisi.

Alisema barabara hizo zinapitika na kwenye maeneo ya vijijini ambako ndio kuna shughuli nyingi za uzalishaji ikiwamo kilimo cha mazao mbalimbali.

Aliwataka makandarasi walioshika tenda hizo kufanya kazi kwa uaminifu na kwa kuzingatia muda ambao upo kwenye mikataba ya miradi hiyo ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.





# Wenyeviti kamati za maafa wapewa jukumu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WENYEVITI wa kamati za maafa za wilaya pamoja na wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri, wametakiwa kusimamia na kutekeleza vyema maagizo na maelekezo ya kanuni za afya yanayotolewa na serikali kuu ili kuziweka salama jamii wanazosimamia katika maeneo yao.

Kufanya hivyo kutaisaidia serikali kuu mikakati inayojiwekea ya kuwalinda wananchi wake hasa wakati huu wa mapambano dhidi ya kudhibiti na kuzuia kuenea kwa virusi vya corona vinavyo sababisha homa ya mafua makali na mapafu.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaabani Seif Mohamed, alisema hayo katika kikao maalumu cha wenyeviti wa kamati za kukabiliana na maafa za wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri kutoka wilaya zote za Zanzibar, mjini hapa.

Shaaban alisema viongozi hao lazima waachane na tabia ya muhali wakati wakitimiza wajibu wao wa kazi kwa kusimamia njia za kuingia nchini ikiwamo bandari rasmi na bandari bubu ili kupambana na viashiria mbalimbali vinavyoweza kusababisha kuenea kwa maambukizo ya virusi vya corona pamoja na kuzuia mikusanyiko ya watu isiokuwa ya lazima.

Katibu Mkuu Shaaban, alisisitiza kauli iliotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuwataka wananchi kuacha tabia ya ukaidi kutekeleza maagizo na miongozo ya serikali inayotolewa kupitia Wizara ya Afya ili kuepuka madhara ambayo tayari yameshaathiri baadhi ya mataifa duniani. Alisema endapo wananchi watapuuza maagizo yanayotolewa na serikali, kuna uwezekano wa kutokea kwa ongezeko la maambukizi ya virusi vinavyosababisha homa ya mafua makali na kusababisha nchi kukumbwa na taharuki na serikali kuchukua uamuzi mgumu.

Naye Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya kukabiliana na maafa Zanzibar, Muhidini Ali Muhidini, akiwasilisha maagizo yaliotolewa na serikali kupitia Kamisheni ya kukabiliana na maafa alisema, wenyeviti wa Kamati za Maafa Wilaya na wakurugenzi wa wilaya wana jukumu kubwa la kuhakikisha mikusanyiko ya watu isiyo ya lazima kwenye maeneo yao inaepukwa wakati huu wa kipindi cha mpito wa janga hilo.

Wakiwasilisha taarifa ya mwenendo wa maradhi ya corona, maofisa kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Halima Ali Khamis na Yahya Mbwana Mselem, walisema Wizara ya Afya inaendelea na utaratibu wa kuwasimamia na kuwafuatilia watu walio katika karantini na jumla ya watu 182 wameruhusiwa baada ya kumaliza muda wao kuwa katika kipindi cha uangalizi.

Wakichangia, wenyeviti wa kamati za maafa pamoja na wakurugenzi wa wilaya, walisema kutokana na ongezeko la maambukizi kuenea ndani ya nchi, ipo haja kwa wananchi wenyewe kuchukua tahadhari na serikali kuweka utaratibu maalumu wa kuwaweka karantini watu wanaotoka maeneo mengine kwa shughuli mbalimbali ikiwamo uvuvi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Muhammed Aboud (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti wa wafanyabiashara wazalendo wa kupambana na Corona, Abdulswamad Abdulrahim (aliyevaa mask), kabla ya kukabidhiwa vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, vilivyotolewa na wafanyabiashara hao, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Bei za petroli, dizeli Zenji zashuka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imefanya mabadiliko ya bei za mafuta zilizoanza kutumika rasmi April 7, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake Maisara, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano, Khudhaimat Bakar Kheir, alisema mafuta ya petroli yatauzwa kwa Sh. 2,110 mwezi huu kutoka Sh. 2,225 ya mwezi uliopita.

Alisema mafuta ya dizeli yameshuka kutoka Sh. 2,260 kwa lita hadi kufikia Sh. 2,098 kwa mwezi huu.

Kwa upande wa mafuta ya taa, Khudhaimat, alisema bei ya reja reja ya mafuta ya taa kwa mwezi huu imefikia Sh. 1,509 kwa lita kutoka Sh. 1,701 kwa lita ya mwezi uliopita.

Akizungumzia mafuta ya meli (Banka), alisema mafuta hayo yamepungua na kufikia Sh. 1,926 kwa lita mwezi huu ikilinganishwa na Sh. 2,086 kwa mwezi uliopita.

Alisema kushuka kwa bei za mafuta kwa mwezi huu kunatokana na kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Aliwaomba wananchi kuwa bei zilizotangazwa na serikali ndio halali na kuwasisitiza kununua mafuta katika vituo halali ili kuepuka kuuziwa mafuta kimagendo au yasiyo salama kwa vyombo vyao.

# Kamati yaridhishwa na juhudi za Dk. Shein

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, imeelezea kuridhika na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuwaendeleza vijana nchini.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo, kuhusu utekelezaji wa maagizo na ushauri unaotokana na ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi mwaka 2019/2020, Mjumbe wa Kamati, Mwanaidi Kassim Mussa, alisema kamati hiyo inaendelea kumpongeza Dk. Shein kwa juhudi kubwa anazozichukua pamoja na kuumwa na kukereketwa na maendeleo ya vijana nchini.

Alisema, jitihada hizo zinaonyesha ni jinsi gani serikali inavyoumwa na maendeleo ya vijana na kuwataka wote waliopewa dhamana ya kuwasimamia kutekeleza wajibu wao. "Tunaendelea kuthamini sana juhudi hizo na tunazidi kuwaomba wote waliopewa dhamana ya kusimamia masuala ya vijana kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais, ili malengo yaliyokusudiwa katika kuwaendeleza vijana wetu yaweze kufikiwa." alisema.

Mapema akiwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Kamati, Waziri wa Wizara ya Vijana, Utamaduni , Sanaa na Michezo, Balozi Ali Abeid Karume, alisema serikali imeunda kamati ya kitaalamu ya kufanya mapitio ya kina ya mradi mzima wa vijana wa pilipili hoho ili kurekebisha kasoro mbalimbali zilizojitokeza na hatimaye kuwasilisha mapendelezo yatakayowezesha kutekeleza mradi huo kwa ufanisi zaidi. Alisema kamati hiyo inaendelea kufanya kazi yake vizuri na itawasilisha mapendekezo yake ya kurekebisha upungufu uliopo baada ya kukamilisha kazi hiyo.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo, Hamza Hassan Juma, aliishauri serikali kuzidi kumuenzi Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Hayati Abeid Aman Karume, kwa kuimarisha miundombinu ya michezo hasa katika kiwanja cha Amani.

Alisema kiwanja hicho ni miongoni mwa matunda ya Mapinduzi matukufu ya 1964, hivi sasa kinapoteza haiba yake hivyo ni vyema kikaendelezwa.

Alisema licha mazingira ya ndani ya kiwanja kuwa sio muafaka, pia maeneo ya nje yamekuwa yakitumiwa vibaya kwa shughuli ambazo hazihusiani na masuala ya michezo.

Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, Ali Khamis Bakari, ameishauri wizara kukamilisha ujenzi wa viwanja vitano vya wilaya ili kukamilisha ahadi inayotokana na Ilani ya CCM ya kukamilisha viwanja hivyo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Kuhusu ushauri na maagizo ya kamati kwa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Waziri wa wizara hiyo, Mahmoud Thabiti Kombo, alisema wizara yake itaendelea kuyafanyia ukarabati magofu na maeneo ya kihistoria awamu kwa awamu ikiwa ni njia mojawapo ya kuyaendeleza maeneo hayo.

Alisema maeneo hayo yamebeba utajiri wa historia kubwa kwa Zanzibar, hivyo ni vyema yakaendelezwa kwa faida ya vizazi vya sasa na baadaye.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


**IN THE DISTRICT DELEGATE OFDODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATIONCAUSE NO…2020**
**In the matter of the Estate of the LATE FRIDOLIN STEVEN MNONJELA OF MIYUJI DODMA CITY**
**And**
**In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by SHORAFIA ROMANUS GODIAT**

**CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 13 of May 2020.

Dated at…this day of….2020

SHorafia
PETITIONER

Presented for filling this Day of April 2020

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY: THE PETITIONER

156971

**TANGAZO**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya: MOSHI MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NO: 38 /2020**

Ombi la **ABDUL RAJABU KIMARO (2) ABDILAH R. KIMARO (3) RASHID R. KIMARO.**

Usimamizi wa mairathi ya marehemu RAJABU SELEMAN KIMARO

**Kwa: YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/4/2020. Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 24/3/2020

115697002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;98/2020**

Ombi la REHEMA NELSON MFUPA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NELSON ISRAEL MFUPA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/04/2020.

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA**

**ABDALLAH MUSSA KAPANGA** AMBAYE NI MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MUSSA KAPANGA MKAZI WA MJINI KATI MANISPAA YA SHINYANGA. ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA NAMBA 31KITALU "G" MJINI KATI MANISPAA YA SHINYANGA, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2019 MAENEO YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA ABDALLAH MUSSA KAPANGA KWA SIMU NAMBA 0763385598.

**RB NAMBA SHY/RB/2020,**
**CONTROL NAMBA 991081234315.**


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Liberia yaagiza raia wake kubaki nyumbani siku 14

**MONROVIA,** Liberia

RAIS wa Liberia, George Weah, ametangaza hali ya dharura kutoka mikoa kadhaa, ikiwa ni pamoja na mji mkuu Monrovia, wananchi wakitakiwa kubaki nyumbani, katika kupambana na kuenea kwa ugonjwa wa virusi vya corona

Rais Weah ambaye ni nyota wa zamani wa mpira wa miguu, ambaye yuko madarakani tangu Januari 2018, alitangaza kwamba ni marufuku kusafiri kati ya majimbo 15 za nchi hiyo.

Katazo hilo litaanza kutekelezwa kuanzia leo majira ya saa 6:00 usiku.

Kutokana na katazo hilo, Kampuni zote na kazi za serikali zisizo muhimu zitafungwa kuanzia muda huo.

Wakazi kutoka majimbo manne ikiwa ni pamoja na Monrovia (yenye wakazi karibu milioni moja), watalazimika kubaki nyumbani kwa wiki mbili, rais wa Liberia alieleza.

Katika kipindi hiki, mtu mmoja tu kwa kila familia ataruhusiwa kutoka, karibu na eneo la makazi yake, kununua chakula au kwa sababu za matibabu, na kwa muda usiozidi saa moja.

"Lazima tujiulize kwa nini tunapaswa kuheshimu hatua hizi. Jibu ni rahisi: kuokoa maisha ya watu," alisema Rais Weah.

Hatua hizi mpya zinakuja kuongezea nguvu hatua zingine ambazo zilichukuliwa hivi karibuni, kama vile marufuku ya mikusanyiko na kuzifungia ndege kutoka nchi zilizoathiriwa na ugonjwa wa virusi vya corona kuingia nchini Liberia.

Kama ilivyo katika nchi zingine za Kiafrika, wataalamu wana hofu kwamba mfumo wa afya hautaweza kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa huo kwa wakazi karibu milioni 4.8, ambao wengi wao wanaishi katika hali ya umaskini.

Nchi hiyo, ambayo inaendelea kuimarisha uhusiano wa karibu na Marekani, imetangaza matukio 13 ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona na vifo vitatu.

Hata hivyo, Rais Weah alibaini kuwa Liberia inakabiliwa na tishio kubwa zaidi tangu kuzuka kwa janga la ugonjwa wa ebola lililoua zaidi ya watu 4,800 kati ya mwaka 2014 na 2016.

RFI



Ugonjwa wa virusi vya corona umeendelea kuiathiri nchi ya Somalia, ambayo inaendelea kukumbwa na mashambulizi ya wanamgambo wa Al Shabab. **PICHA: REUTERS**.

# WHO: Tusilete siasa kwenye janga la corona

**WASHINGTON,** Marekani

MKUU wa Shirika la Afya duniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus, ametaka kuwapo kwa umoja katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona huku shirika hilo likiendelea kushambuliwa na Rais wa Marekani, Donald Trump.

Akizungumza juzi, Ghebreyesus alitetea kazi ya shirika hilo na kutoa wito wa kusitishwa kwa siasa katika mlipuko wa virusi vya corona.

"Tafadhali umoja katika ngazi za kitaifa , tusitumie ugonjwa wa virusi vya corona kisiasa.Tuwe na uaminifu na umoja. Na uongozi wa uaminifu kutoka Marekani na China," alisema Ghebreyesus na kuongeza: "Vitu muhimu vipewe kipaumbele na tafadhalini wekeni siasa karantini," alisema Ghebreyesus.

Rais Trump alionya kwamba atafikiria kusitisha ufadhili dhidi ya shirika hilo la Umoja wa Mataifa baada ya kulishutumu shirika hilo kupendelea China na kudai kwamba walilisaidia sana taifa hilo.

Lakini Dk. Ghebreyesus alipinga matamshi hayo na kusema: "Tunasaidia kila taifa, hatuna upendeleo wowote".

Baada kulishutumu WHO, Rais Trump aliimarisha upya ukosoaji wake katika mkutano na wanahabari siku ya Jumatano akisema kwamba shirika hilo linatoa kipaumbele masuala yake muhimu.

Alisema Marekani itafanya utafiti kuamua iwapo itaendelea kutoa ufadhili wake. Pia akijibu maswali katika mkutano huo na vyombo vya habari Waziri wa mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisema kwamba utawala wa Rais Trump utaangazia upya ufadhili kwa shirika hilo.

"Mashirika lazima yafanye kazi. Lazima kazi zao zionyeshe matunda," alisema Pompeo.

Mshauri wa mkuu wa WHO, alisema kwamba ushirikiano wao wa karibu na China ulikuwa katika kuelewa ugonjwa huo katika hatua zake za kwanza.

Shambulio la Rais Trump dhidi ya WHO limetokea wakati ambapo alikuwa akiukosoa utawala wake kwa jinsi unavyolichukulia janga hilo nchini Marekani.

Mwanzoni mwa wiki, Rais Trump alisema kwamba WHO lilionekana kupendelea China.

Marekani ni mojawapo ya wafadhili wakuu wa kujitolea huku data ya WHO ikionyesha kwamba wanafadhili asilimia 15 ya jumla ya bajeti yote ya shirika hilo. **BBC**

# Sanders ajiondoa kinyang'anyiro urais Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

SENETA Bernie Sanders, amejiondoa katika kinyang'anyiro cha urais, huku akiahidi kushirikiana na Joe Biden, ambaye anapewa nafasi kubwa ya kushinda katika kura za mchujo katika chama cha Democratic.

Sanders aliwaambia wafuasi wa chama chake cha Democratic kushikamana vilivyo kwa kumshinda Rais Donald Trump katika uchaguzi wa urais ambao umepangwa kufanyika Novemba.

Katika kuwatangazia wafuasi wake kwamba anajiondoa katika kura za mchujo za chama cha Democratic, Sanders amemsifu Joe Biden kama mtu anayeheshimika sana na kutangaza kwamba atashirikiana na mgombea mwenye msimamo wa wastani ili kuendeleza mpango wake uliozimwa na mrengo wa kushoto.

Baada ya kuelewa kuwa kuna mivutano kati ya kambi hizo mbili, Makamu wa zamani wa Rais wa Marekani, Joe Biden, mwenye umri wa miaka 77, aliamua kuungana haraka na wafuasi wa Sanders mwenye umri wa miaka 78.

"Najua mtanipigia kura. Na najua inaweza kuchukua muda. Lakini nataka mjue kuwa ninawaona, ninawasikia, na kwamba ninaelewa kwa haraka mnachokitaka, Natumai utajiunga nasi. Tunakuhitaji" alisema Biden, ambaye atachuana na Donald Trump Novemba 3, 2020.

Licha ya kutambua kwamba Biden atakuwa mgombea mteule wa Chama cha Democratic ili kumuangusha Rais Donald Trump katika uchaguzi wa urais, Sander ametangaza kwamba ataendelea kuchuana katika kura za mchujo zilizosalia ili kukusanya wajumbe zaidi ambao watamruhusu kutoa ushawishi mkubwa katika programu ya chama wakati wa mkutano wa Chama cha Democratic utakaofanyika Agosti.

"Kwa pamoja, kwa kuungana, tutamshinda Rais Donald Trump, hatari zaidi katika historia ya kisasa ya Marekani, ameongeza katika hotuba iliyorushwa mtandaoni kutoka nyumbani kwake Burlington, Vermont. RFI



# Besktas yajitosa kumwania Hart

**LONDON,** England

JOE Hart anafikiria kujiunga na Beskitas huku klabu hiyo ya Uturuki ikimrudisha Loris Karius kule Liverpool.

Hart amekuwa na mwaka mwingine mgumu baada ya kucheza mechi mbili tu pale Burnley msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amekuwa na kiwango kibovu tangu alipoondoka Manchester City, lakini tovuti ya Uturuki ya Fanatik imedai Besktas wapo tayari kumchukua.

Tovuti hiyo iliripoti kwamba, Karius anakaribia kurudi Liverpool baada ya kushindwa kung'ara kwa kipindi alichocheza kwa mkopo, tofauti na ilivyotarajiwa.

Na sasa Beskitas wanapanga kumchukua Hart akiwa mchezaji huru wakati mkataba wake na Burnley utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kipa huyo namba moja wa zamani wa England aliondoka City mwaka 2018 na alijiunga na Burnley kwa ada ya pauni milioni 3.5 baada ya kucheza kwa mkopo kule Torino na West Ham.

Hart aliondolewa pale Etihad wakati Pep Guardiola alipochukua mikoba ya kuinoa klabu hiyo mwaka 2016, lakini ameshinda mataji matano akiwa pale.



# Barcelona hawana mpango na Willian

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona, imeripotiwa kuachana na mpango wa kutaka kumsajili, nyota wa Chelsea, Willian, kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Winga huyo wa kimataifa wa Brazil, anakaribia kuondoka pale Chelsea Juni 30, mwaka huu, baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na atakuwa mchezaji huru.

Willian alitaka mkataba wa miaka mitatu na aliondoka kwenye majadiliano hayo wakati Chelsea wakiwa wanapanga kumpa ofa ya mwaka mmoja wa kuongeza mkataba wake.

Wakala wake, Kia Joorabchian, ambaye pia alikuwa mwakilishi wa Philippe Coutinho, tayari alibainisha kwamba mchezaji wake amepata sehemu mpya ya kwenda na kwa mujibu wa Daily Sport, Barcelona imejitoa kwenye mbio hizo.

Miamba hao wa Katalunya awali walikuwa tayari kutoa pauni milioni 50 mwaka 2018 kwa ajili ya kupata huduma yake.

Hata hivyo, kwa sababu hivi sasa kipaumbele chao ni kuwasajili Neymar na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martínez kwa ajili ya msimu ujao.

Na kwa kuwa Willian ana umri wa miaka 31 na anataka mkataba wa miaka mitatu na mshahara mkubwa, Barcelona sasa wameachana na mpango huo na wanawekeza nguvu zao kusajili wachezaji vijana.

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Sadio Mane, amebainisha kwamba angeweza kutua kwa wapizani wao wakubwa Manchester United kabla ya kukamilisha usajili pale Anfield kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 30 akitokea Southampton mwaka 2016.

Mane ameifanya Liverpool chini ya kocha, Jurgen Klopp kuwa ya kiwango cha aina yake na kupaa daraja la juu.

Imetinga mara mbili mfululizo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kulitwaa msimu uliopita, huku sasa wakikaribia kutwaa Kombe la Ligi Kuu kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Hata hivyo, uhamisho wa kujiunga na Liverpool ulikuwa mezani miaka minne iliyopita, lakini yeye na wakala wake walikuwa wanawafikiria zaidi mashetani wekundu.

Alipoulizwa kama usajili wake wa kutua Liverpool ulitarajiwa, Mane aliliambia gazeti la The Times: "Hapana kwa uhakika kabisa. "Tulikuwa tunaifikia zaidi Manchester United.

"Ulikuwa wakati mgumu kwangu, nilikuwa benchi na sikufikiria mtu yeyote angeniita mimi, lakini nilifurahishwa na yeye (Klopp) kuniita kwani hakufikiria kama mimi nitatua hapa."



# Mane afunguka alivyokuwa anaiwaza Man United

## HABARI MICHEZO

# Neymar ni mrithi sahihi wa Messi – Mazinho




**BARCELONA,** Hispania

NEYMAR ni "mrithi sahihi" wa Lionel Messi na angependa kurudi Barcelona, kwa mujibu wa mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na kikosi cha Brazil, Mazinho.

Neymar mchezaji wa kimataifa wa Brazil, aliondoka pale Camp Nou kwa ada iliyoweka rekodi na kujiunga na Paris Saint-Germain kuelekea msimu wa 2017-18 lakini mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Barca.

Licha ya kuhusishwa sana kuondoka msimu wa 2019/20, Neymar alibakia katika mji mkuu wa Ufaransa na amefunga mabao 18 katika mechi 22 kwenye mashindano yote msimu huu.

Neymar kwa mara nyingine tena amehusishwa na mpango wa kujiunga na Barca, ingawa ilisemwa kwamba uamuzi wake wa kuondoka klabuni pale ilikuwa ni kukimbia kivuli cha mchezaji mwenzake na mshindi mara sita wa Ballon d'Or, Messi.

Lakini Mazinho anahisi kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 yupo tayari kurudi na kuchukua nafasi ya Messi kama mtu muhimu wa Barca.

Akizungumza na redio Marca, alisema: "(Barcelona) itakuwa na furaha kama akirudi kesho.

"Yeye ni mrithi sahihi wa Messi. Hakuna mwingine wa kumrithi Messi."

Mazinho ambaye alikuwa kwenye kikosi cha Brazil kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 1994 ni baba wa Thiago Alcantara anayecheza katika Klabu ya Bayern Munich.

## Bayern, Dortmund zamwania Rudiger

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich na Borussia Dortmund zote zimetajwa kumwania beki wa Chelsea, Antonio Rudiger.

Rudiger ameripotiwa kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na Chelsea, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 pia amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Stamford Bridge.

Sky Sports imeripoti kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani anafanya majadiliano kuhusu mkataba wake mpya wa miaka mitatu, ambao pia unahusisha kipengele cha mwaka mmoja zaidi.

Rudiger, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2022, alikuwa na wakati wa kuvutia pale Chelsea kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Ameichezea mechi 16 Chelsea msimu huu, akifunga mabao mawili, ambapo amefikisha jumla ya mabao sita kwenye mechi 105 alizocheza tangu alipotua hapo kwa ada ya pauni milioni 31.5 akitokea AS Roma mwaka 2017.




# Haaland: Sihami kwa kukurupuka




**DORTMUND,** Ujerumani

NYOTA wa Borussia Dortmund na aliyekuwa anawaniwa na Manchester United, Erling Haaland, amebainisha nini anachokiangalia kwenye klabu wakati anapofikiria uhamisho mpya.

United iliachana na mpango wa kumsajili fowadi huyo Januari mwaka huu baada ya kukataa kumpa thamani ya shea katika usajili utakaofuata wakala wake, Mino Raiola na baba yake, Alf Inge Haaland.

Raia huyo wa Norway, alifunga mabao 12 katika mechi 11, ukijumlisha na mabao 28 aliyoyafunga wakati akiwa Red Bull Salzburg nusu ya kwanza ya msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 alimtaja kocha wa zamani wa timu ya taifa ya vijana ya Norway chini ya umri wa miaka 21, Tor Ole Skullerud, kama ndiye mtu mwenye ushawishi zaidi kwake.

"Ni kile Tor Ole anachosema kwangu kuwa muda ni kila kitu." alisema Haaland akiambia Eurosport.

"Unatakiwa kuangalia namna gani ulivyo katika kiwango chako na jinsi klabu ilivyo, watu wa pale, namna gani wanavyokulea, na jinsi wanavyoweza kukusaidia."

Dortmund walikamilisha usajili wa pauni milioni 18 kumsajili Haaland Desemba, mwaka jana, huku akikubali kulipwa mshahara wa pauni 130,000 kwa wiki.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED, ARSENAL ZAMWANIA TOLISSO

●●● Saini ya kiungo huyo Mfaransa inawindwa pia na vigogo wengine wa Ulaya wakiwamo Juventus...

**MANCHESTER,** England

ARSENAL na Manchester United, zinatarajiwa kuanza mchakato wa kumsajili nyota wa Bayern Munich, Corentin Tolisso, mara dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa.

Mfaransa huyo ameshindwa kuonyesha uwezo wake vizuri chini ya Hansi Flick, akiwa ameanza katika mechi saba tangu kocha huyo mpya alipotua kwenye Uwanja wa Allianz Arena.

Kwa mujibu wa gazeti la Foot Mercato, klabu zote mbili, Arsenal na United zinahitaji kujiimarisha kwa kusaka wachezaji watakaowasaidia, na kiungo huyo anatajwa anajipanga kuondoka Bayern na anahitaji kupata changamoto mpya.

Klabu hizo mbili zinazoshiriki Ligi Kuu England, zinatakiwa kujiandaa kupambana na vigogo wengine wa Ulaya, wakiwamo Juventus, Atletico Madrid na Napoli katika vita ya kuwania saini ya Mfaransa huyo.

Taarifa kutoka Ufaransa zinaeleza vigogo wa Bundesliga wako tayari kumwachia Tolisso, ambaye walimsajili mwaka 2017 kutoka Lyon kwa dau la pauni milioni 37.

Tolisso alimaliza muda wake mgumu ndani ya Bayern, kabla Flick, hajatua katika klabu hiyo, na yeye kusumbuliwa na majeruhi.

**Tangu nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 alipotua Bayern miaka mitatu iliyopita, amefanikiwa kucheza mechi 68, amefunga mabao 14 na ametoa pasi za mwisho 12.**

Nyota huyo anatarajiwa kuongeza ubunifu ili atakapojiunga na Arsenal au United, kuzifanya timu hizo kutumiza malengo yake ya kumaliza katika nafasi nne za juu.

Arsenal chini ya Mikel Arteta wanajipanga kurejesha heshima ya klabu yao kwa kuimarisha safu hiyo ya kiungo ifikapo dirisha la usajili la majira ya joto, wakati United mbali na kuijenga timu, inataka kuhakikisha inapata mrithi wa Mfaransa Paul Pogba atakapoondoka kwenye klabu hiyo.

Klabu hizo mbili zinemwania Tolisso ambaye alionyesha kiwango kizuri na aliisaidia Timu ya Taifa ya Ufaransa kutwaa Kombe la Dunia katika fainali zilizopita ambazo zilichezwa mwaka juzi.

The Gunners pia watapambana na United katika vita nyingine ya kuwania saini ya kiungo wa Real Madrid, James Rodriguez.

Kwa mujibu wa gazeti la AS la Hispania, limeandika huenda Rodriguez akatumika kama sehemu ya mchakato wa usajili wa Pogba, ambaye anatakiwa zaidi na Kocha wa Los Blancos, Zinedine Zidane.

Rodriguez ambaye ni nyota wa kimataifa wa Colombia ambaye ana umri wa miaka 28, ameichezea Madrid mechi saba za La Liga msimu huu, na amekuwa pia akihusishwa kutakiwa na Everton, Napoli na Juventus.

## KWA UFUPI

### CHELSEA YAMTAKA COUTINHO

CHELSEA wako katika mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho. Nyota huyo wa zamani wa Liverpool mwenye umri wa miaka 27 kwa sasa yuko kwa mkopo Bayern Munich. (Sport)

### UNITED, NAPOLI VITANI

MANCHESTER United na Napoli wameonyesha nia ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28). (AS, in Spanish)

### GREALISH BADO AWINDWA

KIUNGO mchezeshaji wa Aston Villa, Jack Grealish (24), bado anatajwa ni mmoja wa wachezaji wanaotakiwa na Manchester United katika dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa. (Evening Standard)

### BARCA YAMWACHA WILLIAN

BARCELONA imepoteza matumaini ya kunasa saini ya mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Brazil, Willian, licha ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 kupatikana kama mchezaji huru ifikapo mwishoni mwa msimu huu. (Sport)

### RUDIGER, CHELSEA WATETA

MABOSI wa Chelsea wameanza mazungumzo na Antonio Rudiger. Klabu hiyo ina mkakati wa kunasa saini ya nyota huyo na kumpa mkataba mrefu utakaomalizika ifikapo mwaka 2023. (Sky Sports)

### HART ANUKIA BESIKTAS

BESIKTAS imeanza mazungumzo ya kumsajili golikipa wa Burnley na timu ya Taifa ya England, Joe Hart (32), ili kuziba pengo litakaloachwa na Mjerumani Loris Karius (26), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Liverpool.(Fanatik, in Turkish)

### CARLOS AFURAHIA SEVILLA

BEKI Diego Carlos (27), amesema anafurahi kuendelea kuitumikia Sevilla licha ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na Liverpool. Ada ya kumnunua Mbazili huyo ambayo imewekwa katika mkataba wake ni pauni milioni 64. (Estadio Deportivo, in Spanish)

### MANE AITAJA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Senegal, Sadio Mane (27), amesema alitarajia kujiunga na Manchester United kabla ya kutua Anfield. (Times, subscription required)

### CORONA KUMTESA MBAPPE

REAL Madrid itachelewa kuanza mchakato wa kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe (21), kutoka Paris Saint-Germain mpaka itakapofika mwaka 2021 kwa sababu ya kuwapo kwa janga la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. (AS)

### SOUMARE ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imejiunga kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo wa Lille, Boubakary Soumare (21). Klabu nyingine ambazo tayari zinamwinda nyota huyo Mfaransa ni pamoja na Real Madrid, Manchester United, Chelsea na Newcastle. (Sport)

### SILVA ATAKIWA MILAN

MABOSI wa AC Milan wameanza mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Manchester City, David Silva. Nyota huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania anatarajia kumaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu. (Corriere Dello Sport - in Italian)

# GWAMBINA FC YAKIMBIA 'KIVULI' CHA SIMBA, YANGA

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha kikosi chake kinaendelea kuonyesha ushindani, Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, amesema katika usajili wake hatakuwa na mpango wa kusajili wachezaji 'watakaotemwa' na vigogo wa soka nchini, Simba, Yanga na Azam FC.

Gwambina FC inakaribia kupanda daraja baada ya kufanya vema kwenye kundi lake katika mechi za Ligi Daraja la Kwanza ambayo nayo inaelekea hatua ya lala salama.

Akizungumza na gazeti hili jana, Novatus alisema ataongeza nguvu katika kikosi chake lakini ataelekeza kusaka wachezaji kutoka timu za nje ya Dar es Salaam ambao anaamini wataisaidia timu yake kufanya vema kwenye msimu ujao katika Ligi Kuu Bara.

Novatus alisema timu yake inataka kutoa ushindani hivyo atasajili wachezaji ambao bado wanahitaji kutimiza ndoto zao.

"Nitaangalia wachezaji kutoka Ndanda, KMC, Mbao au timu nyingine za chini, hawa kutoka timu kubwa sijawapa nafasi katika kikosi changu, sababu kubwa hawana jipya ambalo wataleta ukilinganisha na wengine wanaotoka timu za chini," alisema Novatus.

Kocha huyo alisema kutokana na kikosi chake kuwa na wachezaji wengi vijana, hatarajii kufanya mabadiliko makubwa.

"Ukiangalia kikosi changu kipo imara, ukiangalia timu nilizocheza nazo za Ligi Kuu ikiwamo Simba, Prisons, Mbao na Yanga nazo tulizitoa jasho, walipata changamoto ya ushindani na timu hizo," Novatus alisema.

Aliongeza kwa kutaja siri ya mafanikio ya kikosi chake kuwa ni nidhamu na kuwasisitiza wachezaji wajitume ili watimize ndoto zao na si kuishia kusindikiza wengine.



Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo (katikati), akimkabidhi mipira, Abdallah Kibadeni (kushoto), na Sunday Manara kwa ajili ya kuendeleza soka la vijana katika vituo walivyofungua hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

## Gullit aiwaza Ligi Kuu Bara

**Na Hawa Abdallah, Zanzibar**

ALIYEKUWA kuwa Kocha Msaidizi wa Stand United ya Shinyanga, Khamis Gullit, amesema anategemea kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao wa mwaka 2020/21, imefahamika.

Hata hivyo Gullit hakuwa tayari kutaja ni klabu ipi ameanza kufanya mazungumzo nayo kwa lengo la kuifundisha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gullit alisema ni mapema kuitaja timu ambayo anatarajia kuifundisha kwa sababu mazungumzo yako katika hatua za awali.

"Natamani kurudi tena Bara kufundisha timu ambayo itapata mafanikio makubwa katika soka, hii ndiyo ndoto niliyonayo kwa sasa na ninaamini itatimia," alisema Gullit.

Aliongeza sababu mojawapo inayomfanya akumbuke timu za Bara ni maslahi bora wanayopata makocha ukilinganisha na mishahara wanayolipwa na klabu za Zanzibar.

Alisema pia miundombinu kwa upande wa Bara ni mizuri na hii huwafanya makocha kutekeleza majukumu yao kwa urahisi.

## Itigi yakaribia kupata viwanja

**Na Jumbe Ismailly, ITIGI**

AWAMU ya pili ya ujenzi wa viwanja vya michezo mbalimbali vinavyomilikiwa na Hospitali ya Mtakatifu Gasper iliyopo Itigi, mkoani Singida imeanza kutekelezwa kwa kuweka nyasi bandia kwenye eneo la kiwanja cha mpira wa miguu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Padri Serafini Lesiriani, alisema ujenzi wa uwanja huo ulianza tangu mwezi uliopita na mchakato wa kuweka nyasi bandia unaelekea katika hatua za mwisho.

Lesiriani alisema katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa viwanja vya mpira wa kikapu, pete na wavu ilivyotumia Euro 45,000.

Aliwaita wakazi wa Itigi kujitokeza kufanya mazoezi ambayo yatasaidia kuimarisha miili yao na vile vile kujikinga na maradhi.

Wakati huo huo, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Singida inatarajia kujenga uwanja wa mpira wa wavu utakaogharimu Sh. milioni tano katika kipindi cha mwaka wa 2020/21.

# Mahadhi awatuliza mashabiki Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukaa muda mrefu nje kwa sababu ya kuwa majeruhi, mshambuliaji wa Yanga, Juma Mahadhi amesema ana 'deni kubwa' na klabu hiyo ambayo ilimsajili akitokea Coastal Union ya jijini Tanga.

Mahadhi aliliambia gazeti hili atakapofanikiwa kurejea uwanjani, atapambana kuhakikisha anawapa furaha mashabiki wa Yanga ambao walitarajia kumuona akiisaidia timu kwenye mashindano mbalimbali.

Nyota huyo alisema anaahidi kuendeleza ushindani katika kikosi hicho na kuisaidia Yanga kutimiza malengo yake ya msimu ujao.

"Nina deni kubwa kwa mashabiki wangu pindi Ligi Kuu itakaporejea, nitalipa deni hilo kwa kuendeleza kasi niliyokuwa nayo," alisema Mahadhi.

Alieleza kwa sasa ameshaanza kufanya mazoezi magumu kwa kufuata programu maalumu aliyopewa na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mholanzi Hans van der Pluijm.

"Nafanya mazoezi magumu kuuweka sawa mwili wangu ili kujiandaa na ligi, ninaamini Mungu atanisimamia na kurejea katika kiwango changu," Mahadhi alisema.

Aliendelea kuishukuru Yanga kwa kumpa huduma zote muhimu tangu alipoanza kuumwa na madaktari wanaofuatilia afya yake kwa karibu.

"Ninashukuru ninapata ushirikiano mkubwa kutoka katika klabu yangu, mpaka hapa nilipo sasa siwezi kuisema vibaya timu yangu, wanasimamia huduma zote ninazotakiwa kupata za hospitali," Alisema Mahadhi. Mahadhi aliuimia katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa kati ya Yanga dhidi ya TP Mazembe hapo mwaka juzi na usajili wake ulitarajia kuziba pengo la Simon Msuva ambaye baadaye alijiunga na klabu ya Difaa El Jadida ya Morocco.

Michezo
Ijumaa Aprili 10, 2020
Nipashe

## United, Arsenal zamwania Tolisso



HABARI UK.22

# MIHAYO AWATAKA SIMBA KUZINDUKA



Washambuliaji wa Liverpool, Mohammed Salah (kushoto) na Sadio Mane, wakishangilia baada ya mmoja wao kufunga katika mechi ya Ligi Kuu England mapema mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**.

●●● Ni kiongozi aliyeongoza mchakato wa mabadiliko, akumbushia barua ya siri...

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Kamati ya Mabadiliko ya Simba, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, amesema viongozi wa klabu hiyo hawajafuata maelekezo ambayo kamati yake iliekeza baada ya kukamilisha kazi iliyopewa, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mihayo alisema endapo viongozi wa Simba wangefuata maelekezo na ushauri uliotolewa na kamati yake, kusingekuwa na mgongano wowote ndani ya klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Mihayo alisema kamati yake ilikabidhi barua ya 'siri' kwa viongozi wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kama ingefuatwa, sasa kusingekuwa na tatizo lolote ndani ya klabu hiyo.

"Tatizo la viongozi wa Simba hawaelewi nini wanafanya, Sh. bilioni 20 ilikuwa ni kwa sababu ya hisa asilimia 49, baada ya mchakato wa kumpata mwekezaji,... kulikuwa na mambo mengine ya kuiarifu serikali," alisema Jaji Mihayo.

Alitaja moja ya ushauri uliokuwapo kwenye barua hiyo ni maelekezo ambayo Simba ilitakiwa kuiarifu serikali.

> **"Tuliweka vigezo vyetu, vigezo alivifikia, kuna vingine ambavyo vilikuwa vya mchakato na tukawaachia viongozi mhakikishe vigezo hivi 1, 2, 3 vimefikiwa," Mihayo alisema.**

Aliongeza kamati yake ilitumwa kufanya kazi ya kuandaa mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji na kilichoendelea hakikuwa kwenye dhamana yao.

"Baada ya kuandika lile, nilifunga dirisha, kazi yangu niliambiwa kuandaa mchakato wa kumpata mwekezaji ili muundo wa Simba ubadilike kutoka Simba Sports Club iwe Simba Company Limited, hicho ndio nilichofanya," Mihayo alisema.

Naye aliyekuwa Katibu Mkuu wa Yanga, Jonas Tiboroha alisema Simba ilianza mchakato wa mabadiliko hali ya kuwa haijatengeneza mtaji wake halisi.

Tiboroha alisema thamani ya Simba ni zaidi ya Sh. bilioni 200 na asilimia 49 ambayo mwekezaji na mfanyabiashara maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo', amepewa haikuwa sahihi.

"Simba haijui thamani yake, thamani ameitaja Mo, hivi kweli Simba thamani yake ni bilioni 20, mimi kwangu nasema ni zaidi ya Sh. bilioni 200 na hiyo ni thathmini ya haraka haraka," Tiboroha alisema.

Kaimu Mwenyekiti wa Simba, Mwina Kaduguda, alisema jana klabu hiyo inaendelea na mchakato huo wa mabadiliko na anaamini mafanikio watakayopata, yatazivutia klabu nyingine za Afrika Mashariki na Kati.

## Yanga yamtuliza rasmi Tshishimbi

**Na Saada Akida**

HATIMAYE uongozi wa Yanga umefanikiwa kukamilisha mchakato wa kumwongezea mkataba mpya kiungo wake wa kimataifa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Papy Tshishimbi, ambaye inadaiwa alikuwa anawindwa na watani zao, Simba, imefahamika.

Mbali na kukamilisha usajili huo, Yanga pia imemaliza tofauti iliyokuwapo na wadhamini wao, Kampuni ya GSM, baada ya kufikia muafaka katika kikao kilichofanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema Tshishimbi amesaini mkataba mpya wa miaka miwili akiwa ni mmoja wa wachezaji waliopendekezwa kubakia na Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael.

Akizungumza na gazeti hili jana, Tshishimbi alisema amesaini mkataba wa kuendelea kuitumikia Yanga baada ya klabu hiyo kumpatia dau alilowatajia.

"Tayari tumeshamalizana, biashara imekwisha, Wanayanga bado tuko pamoja," alisema kwa kifupi kiungo huyo Mkongomani.

Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Hersi Said, alisema tayari tofauti zilizokuwapo kati yao na Yanga zimemalizika na sasa hivi wanajipanga kuhakikisha klabu hiyo inaimarisha kwa kuanza na mchakato wa usajili.

Said alisema wameanza na Tshishimbi na wanaahidi kikosi cha timu hiyo itakuwa imara ili msimu ujao waweze kuchukua ubingwa wa Tanzania Bara na Afrika.

Aliongeza chini ya GSM, Yanga inajipanga kusajili kikosi kitakachokuwa na uwezo wa kupambana kuwania taji la Afrika kwa kuwapatia wachezaji mahitaji yote muhimu ili wafikie malengo yao.

"Hili suala la kukosa ubingwa mara tatu mfululizo linaumiza sana, hivyo tushirikiane kuhakikisha tunafanya usajili mzuri na huku tukipambana kubakiza wachezaji ambao wamemaliza mkataba na bado wanahitajika," Said aliongeza.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, amewataka wanachama wa klabu hiyo kujiandaa na mfumo mpya wa uwekezaji ambao utaibadilisha klabu hiyo.

Nugaz alisema Yanga itashirikiana na maofisa wa La Liga katika mchakato huo wa mabadiliko ambao utawaondoa kwenye mfumo tegemezi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >